# MIKAKATI YA UPOLE KATIKA *MSTAHIKI MEYA* YA TIMOTHY AREGE

NA

ENDOVU BRAICY INZIANI

TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA MASOMO YA KISWAHILI IDARA YA KISWAHILI, CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2017

## UNGAMO

Nakiri kuwa tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawai kuwasilishwa kwa madhumuni ya shahada yoyote katika Chuo Kikuu kingine.

Sahihi__________________ Tarehe _______________

**BRAICY INZIANI ENDOVU**

(Mtahiniwa)

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioidhinishwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi ______________ Tarehe __________________

**DKT. EVANS MBUTHIA**

(Msimamizi)

Sahihi _____________ Tarehe ____________

**MS. MARY NDUNG'U**

(Msimamizi)

## TABARUKU

Kwenu nyie wazazi wangu wapendwa:

Mamangu Janet Musimbi Endovu na Babangu, Joseph Isaac Endovu mlionielekeza na kunishauri kuhusu namna za kukabiliana na changamoto za maisha.

## SHUKRANI

Ama kwa hakika umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu, mchakato mzima wa kuimaliza tasnifu hii si bidii yangu pekee na haingefanikiwa bila msaada wa wengine. Kwanza kabisa shukrani zangu ni kwa Mola kwa nehema zake na kunipa nguvu za kukabiliana na changamoto mbalimbali wakati nikiitafitia mada hii. Sina budi kukiri kuwa Mwenyezi Mungu amenipatia nguvu na hamu ya kuendelea kuisukuma kazi hii hasa pale nilihisi kulemewa na changamoto za maisha. Kwa msingi huu natangaza kuwa, shukrani, utukufu na heshima ni zake.

Pili, natoa shukrani zangu kwa wasimamizi wangu; Dkt. Evans Mbuthia na Bi. Mary Ndung’u kwa kunielekeza katika kuiandaa kazi hii kuanzia mwanzo hadi mwisho. Kwa hakika, mmenielekeza na kunifunza mengi kuhusu utafiti ambayo isingekuwa nyinyi ingekuwa vigumu kuyaelewa. Asante kwa uvumilivu ambao mmekuwa nao kwangu katika kunikosoa na kunielekeza hadi nikafika kiwango hiki. Shukrani sana na mola awabariki sana.

Vile vile, shukrani teletele ziwaendee wahadhiri wote wa Chuo Kikuu cha Nairobi, idara ya Kiswahili. Maelekezo, mafunzo na ushauri wenu ulinitia motisha na hamu ya kuifanya kazi hii na kuikamilisha. Wahadhiri hawa ni pamoja na; Prof. Iribemwangi, Prof. Habwe, Prof. Kithaka, Prof. Wamitila, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. Abdulaziz, Dkt. Zaja, Dkt. Mukhwana, Dkt. Evans Mbuthia, Bi. Mary Ndung’u, Dkt. Swaleh, Dkt. Mweri, Dkt. Rayya Timmamy na wengine wote.

Mwisho, ningetaka kuwashukuru wanafunzi wenzangu ambao tulianza safari hii nao kwa ushauri na uelekezi wao. Wanafunzi hawa wamekuwa wakinitia motisha na kunipa mawaidha nilipohitaji. Wanafunzi hawa ni pamoja na; Alivitsa Eunice, Winy Owuor, na wengine wengi. Wote nawatambua na kuwapa shukrani kwa ushauri wenu. Mungu awabariki sana.

# IKISIRI

Utafiti huu umeshughulikia suala la upole kama linavyodhihirishwa katika tamathali za usemi na ukuzaji wa maudhui katika tamthilia *ya Mstahiki Meya*. Tumetumia mtazamo wa Nadharia ya Brown na Levinson (1987) hasa kipengele cha mikakati ya upole. Data ya utafiti huu ilitokana na uchambuzi wa matamshi ya wahusika katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Lengo la kwanza la utafiti huu lilikuwa ni kubainisha iwapo tamathali za usemi hudhihirisha upole katika mazungumzo ya wahusika. Matokeo yanadhihirisha kuwa, tamathali za usemi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* zimedhihirisha upole kutoka na namna wahusika wanavyoingiliana. Lengo la pili la utafiti huu lilikuwa kubainisha iwapo upole hudhihirika katika ukuzaji wa maudhui katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Utafiti huu ulidhamiria pia kuchunguza iwapo miktadha mbalimbali ya mazungumzo huchangia kudhihirisha upole. Matokeo yanaonyesha kuwa, matumizi ya mikakati ya upole hudhihirika kupitia miktadha mbalimbali ya mawasiliano. Kwa jumla, utafiti huu umedhihirisha kuwa, upole una nafasi kubwa katika kuimarisha kazi ya tamthilia. Kwa hivyo, ndiposa mawasiliano yakamilike ni lazima viwango na matumizi ya mikakati ya upole ya wahusika yazingatiwe.

# YALIYOMO

UNGAMO ..... ii
TABARUKU ..... iii
SHUKRANI ..... iv
IKISIRI ..... v
YALIYOMO ..... vi
MAELEZO YA ISTILAHI NA VIFUPISHO ..... xi
SURA YA KWANZA ..... 1
1.1 Usuli Wa Mada ..... 1
1.2 Tatizo la Utafiti ..... 6
1.3 Madhumuni ya Utafiti ..... 6
1.4 Maswali ya Utafiti ..... 7
1.5 Sababu za Kuchagua Mada ..... 7
1.6 Upeo na Mipaka ..... 8
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..... 8
1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Upole ..... 8
1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Tamthilia ya Mstahiki Meya ..... 13
1.8 Msingi wa Kinadharia ..... 14
1.10 Mbinu za Utafiti ..... 21
1.10.1 Uteuzi wa Sampuli ..... 21
1.10.2 Ukusanyaji wa Data ..... 21
1.10.3 Uchanganuzi wa Data ..... 21
1.10.4 Uwasilishaji wa Data ..... 22
SURA YA PILI ..... 23
MIKAKATI YA UPOLE KATIKA KUJENGA USHIRIKIANO KATIKA ..... 23

MAZUNGUMZO ........ 23

2.0 Utangulizi ........ 23

2.1 Kanuni za Ushirikiano (Grice, 1975) ........ 23

2.1.1 Kanuni ya Ukweli ........ 23

2.1.2 Kanuni ya Idadi ........ 24

2.1.3 Kanuni ya Uhusiano ........ 24

2.1.4 Kanuni ya Namna ........ 25

2.2 Kanuni za Upole Kulingana na Leech (1983) ........ 26

2.2.1 Kaida ya Ukarimu ........ 27

2.2.2 Kaida ya Kumwonea Huruma Msikilizaji ........ 27

2.2.3 Kaida ya Kujitweza ........ 28

2.2.4 Kaida ya Kumsifu Msikilizaji ........ 28

2.2.5 Kaida ya Makubaliano ........ 29

2.2.6 Kaida ya Mkakati ........ 29

2.3 Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) na Namna Imetumika Kukiuka au Kudhihirisha Upole ........ 30

2.3.1 Vitendo Vinavyotishia Uso ........ 31

2.3.2 Namna ya Kukabiliana na Vitendo Vinavyotishia Uso ........ 32

2.3.2.1 Mkakati Chanya wa Upole ........ 33

2.3.2.1.1 Kutumia Ucheshi ........ 33

2.3.2.1.2 Kutafuta Makubaliano ........ 34

2.3.2.1.3 Kuepuka Kutokubaliana ........ 34

2.3.2.1.4 Kumtambua na Kumshughulikia Msikilizaji ........ 34

2.3.2.1.5 Kuuliza au Kutoa Sababu za Kitendo Fulani ........ 35

2.3.2.1.6 Kutumia Vitambulisho vya Makundi ........ 35

2.3.2.1.7 Kuwa Mrijua ........................................ 35

2.3.2.2 Mkakati Hasi wa Upole ........................................ 35

2.3.2.2.1 Kutumia Maswali na Vidokezo ........................................ 36

2.3.2.2.2 Kutumia Vitangulizi ........................................ 36

2.3.2.2.3 Kuomba Msamaha ........................................ 36

2.3.2.2.4 Kutaja Kanuni ya Jumla ........................................ 36

2.3.2.2.5 Kuonyesha Heshima Baina ya Msemaji na Msikilizaji ........................................ 37

2.3.2.2.6 Kuwa Bila Rajua ........................................ 37

2.3.2.3 Mkakati wa Kuwa Ndani ya Rekodi ........................................ 37

2.3.2.3.1 Katika Hali ya Dharura au Kutamauka ........................................ 37

2.3.2.3.2 Kutoa Ahadi kwa Msikilizaji ........................................ 37

2.3.2.3.3 Tofauti za Kimamlaka Kati ya Msemaji na Msikilizaji ........................................ 38

2.3.2.3.4 Katika Kitendo cha Kumfaidi Msikilizaji ........................................ 39

2.3.2.4 Mkakati wa Kuwa Nje ya Rekodi ........................................ 39

2.3.2.4.1 Kutumia Kejeli au Kinaya ........................................ 39

2.3.2.4.2 Kutumia Vidokezo ........................................ 40

2.3.2.4.3 Kutumia Maswali ya Balagha ........................................ 40

2.3.2.4.4 Kuzua Utata ........................................ 41

2.3.2.4.5 Matumizi ya Sitiari ........................................ 41

2.3.2.5 Mkakati wa Kukabiliana na Vitishio kwa Uso kwa Kutowasilisha Taarifa Kabisa ......... 42

2.4 Hitimisho ........................................ 42

SURA YA TATU ........................................ 43

NAMNA TAMATHALI ZA USEMI ZINAVYODHIHIRISHA UPOLE ........................................ 43

KATIKA TAMTHILIA YA MSTAHIKI MEYA ........................................ 43

3.0 Utangulizi ........ 43
3.1 Majazi ........ 43
3.1.1 Sosi ........ 43
3.1.2 Siki ........ 44
3.1.3 Kheri ........ 45
3.1.4 Cheneo ........ 46
3.2 Sitiari ........ 46
3.3 Maswali ya Balagha ........ 49
3.4 Uhuishi ........ 51
3.5 Methali ........ 53
3.6 Tashbihi ........ 56
3.5 Hitimisho ........ 57
SURA YA NNE ........ 58
UPOLE NA UKUZAJI WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA YA *MSTAHIKI MEYA* ........ 58
4.0 Utangulizi ........ 58
4.1 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kukuza Maudhui ........ 58
4.1.1 Matumizi ya Mkakati Ndani ya Rekodi ........ 58
4.1.3 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Upole ........ 66
4.1.4 Matumizi ya Mkakati Nje ya Rekodi ........ 68
4.2 Hitimisho ........ 69
HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 70
5.0 Utangulizi ........ 70
5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 70
5.2 Hitimisho ........ 71

5.3 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo.......................................................................... 72

MAREJELEO ............................................................................................................. 73

## MAELEZO YA ISTILAHI NA VIFUPISHO

MDR **-** Mikakati ya Ndani ya Rekodi.

MNR **-** Mikakati ya Nje ya Rekodi.

MUC - Mikakati ya Upole Chanya.

MUH - Mikakati ya Upole Hasi.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Usuli Wa Mada

Katika mawasiliano huwa kuna watu wawili au zaidi: mzungumzaji na msikilizaji au wasikilizaji. Mzungumzaji ndiye aliye na jukumu la kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji naye msikilizaji anafaa kutoa maelezo au majibu yake. Pia msikilizaji anaweza kutoa ujumbe fulani kwa msemaji akiitaji ufafanuzi kutokana na mazungumzo yao. Katika shughuli nzima ya kuwasilisha ujumbe ni muhimu kuhakikisha ya kwamba ujumbe umewasilishwa kwa njia ifaayo huku kanuni za upole zikifuatwa au na kukiukwa.

Ni muhimu katika mawasiliano yoyote mtu kuchagua maneno na hata njia mwafaka ya kuwasilisha ujumbe bila kumuudhi anayeupokea ujumbe huo. Mawasiliano yoyote hutumia lugha; iwe ni lugha ishara au lugha ya mazungumzo. Lugha hutumiwa ili kufanikisha ubadilishanaji wa taarifa unaoleta maana baina ya pande mbili au zaidi na walengwa wake, hasa huwa ni viumbe hai. Lugha ya mwanadamu imeundwa katika mifumo ya sauti na maana. Lugha huundwa kwa sauti ambazo huunganishwa kuunda neno au sehemu ya neno. Maneno huungana kuunda miundo mikubwa zaidi yenye maana kama virai, vishazi, sentensi na aya. Huu ndio msingi wa mawasiliano. Kwa hivyo, lugha ya mwanadamu ni mfumo wenye kanuni, sheria na taratibu ambazo zikikiukwa basi mawasiliano yanaweza kukwama. Kanuni hizi zinazotawala katika lugha ndizo zinazowawezesha watumiaji wa lugha fulani kuelewana.

Lugha katika mawasiliano huwa na majukumu ambayo ni: kuendeleza shughuli mbalimbali za kijamii k.v za kibiashara au kiuchumi na kusaidia wanajamii kuingiliana na kuleta utangamano katika jamii. Katika jukumu la kwanza, la kuendeleza shughuli mbalimbali za kijamii, la muhimu huwa ni kufikisha ujumbe muhimu na kuafikia hatima ya jambo fulani kwa mfano kama ni mazungumzo ya hospitalini, daktari na mgonjwa ni lazima waweze kuafikiana kwa njia ya mawasiliano. Daktari atamuuliza mgonjwa amweleze pale anahisi maumivu naye mgonjwa kwa njia iyo hiyo ya mazungumzo amweleze daktari ndiposa atapewa dawa ya kutuliza maumivu.

Katika jukumu la pili la kusaidia wanajamii kuingiliana na kutangamana la muhimu huwa ni kudumisha uhusiano mwema miongoni mwa wanajamii katika jamii husika. Kuna namna ambayo watoto hutumia lugha katika mazungumzo yao na namna watu wazima huwasiliana.

Hata hivyo watoto huwasiliana na watu wazima tofauti na vile wangewasiliana na watoto wenzao.

Mawasiliano huhusisha kupashana au kubadilishana mawazo, maoni au habari kwa maneno, maandishi au na ishara. Ingawa kuna mawasiliano ya njia moja, mawasiliano ni mchakato kati ya msemaji na msikilizaji ambapo kuna mabadilishano ya mawazo au hisia na kukuza kwa fikra, kufikia lengo lililokubaliwa au mwelekeo uliokubaliwa.

Kulingana na Mckenzie (1997), mawasiliano huhitaji kuwa msemaji na msikilizaji wawe na jambo linalowaunganisha kimawasiliano. Kuna njia zinazohusisha kusikia kama vile unenaji, wimbo na toni ya sauti na kuna zile zisizohusisha kusikia kama vile miondoko ya mwili, lugha ishara, kugusa, kuwasiliana kwa macho na kuandika. Mzungumzaji na msikilizaji wanapotumia njia hizi zote wakati wa mawasiliano, ni sharti wafanye hivyo bila kupujuana uso. Mzungumzaji na msikilizaji watawasiliana bila kupujuana uso iwapo watafuata mikakati yote ya upole. La muhimu ni kwamba mawasiliano baina yao yaweze kufikia malengo yake.

Anaeleza kuwa, unapotaka njia inayotumiwa katika kutoa na kufikisha maana katika jaribio la kusababisha ufahamu wa jumla utatumia mawasiliano. Utaratibu huu unahitaji mkusanyiko mkubwa wa ujuzi wa mawasiliano miongoni mwa na baina ya watu, kusikiliza, kutazama, kuongea, kuhoji, kuchambua na kutathmini. Mawasiliano hutokea kupitia kwa ushirikiano. Mawasiliano huwa na vizingiti. Viwili kati yake vikiwa kupasha ujumbe kupita kiasi (mtu anapopokea ujumbe mwingi mno kwa wakati mmoja) na ujumbe changamano. Ujumbe mwingi kupita kiasi kwa wakati mmoja humchanganya msikilizaji.

Kulingana na yeye, ushawishi katika mawasiliano hutegemea msikilizaji na mzungumzaji. Watu huweza kujiwasilisha kwa njia mbalimbali: uso kwa uso, ubavu kwa ubavu au hata wakifuatana. Kwa mfano, watu walio na ushirikiano kuna uwezekano watakaa ubavu kwa ubavu na washindani wakati mwingi hutazamana.

Kutabasamu, kukunja uso, kuinua nyusi, piga miayo na kukenua, hivi vyote huwasilisha habari. Ishara za uso hubadilika mara kwa mara wakati wa mawasiliano na kufuatiliwa sana na mpokeaji. Mawasiliano huweza kuwa na msikilizaji mmoja, kikundi au hata hadhira. Mawasiliano mazuri huchangiwa na neno au ujumbe alionao msemaji. Jinsi unavyowasilisha

ujumbe huwa na athari kubwa kwa msikilizaji. Ni lazima unase umakini wa hadhira na uhusiane nao. Kwa mfano, watu wawili wanaosema kichekesho mmoja wao anaweza kuifanya hadhira kuangua kichako kutokana na miondoko mizuri ya kimwili na toni ya sauti. Hata hivyo mtu wa pili anayewasilisha kichekesho kile kwa maneno yale yale anaweza kuifanya hadhira itazamane.

Mawasiliano kwa kawaida hufafanuliwa kwa kuzingatia mitazamo kama vile; ujumbe unaosemwa, msemaji wa ujumbe huo, aina ya ujumbe, njia inayotumiwa kupitisha ujumbe huo, anayepokea ujumbe huo na lengo la ujumbe huo. Wakati wa kutekeleza mitazamo hii ni vyema msikilizaji na mzungumzaji kuzingatia mikakati ya upole ndiposa waweze kuhifadhi nyuso zao. Ujumbe unaohitajika uweze kumfikia msikilizaji kwa njia inayofaa na lengo lake liweze kutimizwa. Namna ya kutafsiri ujumbe wa msemaji inaweza kuwa tofauti na ya msikilizaji kulingana na desturi na tamaduni za eneo walilomo, au jinsia, mambo ambayo yanaweza kuathiri ujumbe uliokusudiwa.

Katika mawasiliano ni vizuri kuzingatia maadili ya jamii husika ili kuzingatia upole katika mazungumzo. Ili kuweza kuelewa ni mambo gani yanafaa kusemwa bila kumuudhi anayeambiwa ni vizuri kuzingatia mambo k.v mahusiano ya kijamii, matabaka, vyeo, wakati, umri, jinsia, kiwango cha elimu, mahali au mandhari, wahusika na hata tukio lenyewe. Kwa mfano, jamii inatarajia kuwa mtu wa cheo cha juu anafaa kuzungumziwa kwa heshima zaidi akilinganishwa na mtu wa kawaida. Mawasiliano yanayohusisha watu wa vyeo vya juu huwa ni rasmi zaidi ikilinganishwa na wale wa vyeo vya chini. Jambo la mandhari au mahali hutokea kwa vile mawasiliano hutegemea kama ni rasmi au ya kirafiki. Kwa mfano, mawasiliano baina ya mwalimu na mwanafunzi ni tofauti na yale ya wauzaji na wateja. Mwalimu na mwanafunzi watatumia lugha rasmi huku muuzaji na mteja wake watatumia lugha isiyo rasmi.

Jamii pia inachukulia kuwa tajiri anafaa kuzungumziwa kwa heshima zaidi akilinganishwa na maskini ndiposa jambo la utabaka linajitokeza. Hii ni kwa sababu swala la upole ni la kijamii na kila jamii ina mtazamo wake wa upole. Kile ambacho jamii moja inachukulia kuwa ni upole, kinaweza kuwa si upole katika jamii nyingine.

Kwa jumla, katika mawasiliano ni muhimu kuzingatia kanuni za upole ili kuhifadhi heshima ya anayezungumziwa. Hata hivyo kanuni hizi zinaweza kukosa kuzingatiwa kwa lengo lilo hilo.

Msemaji anafaa kuhakikisha kuwa ujumbe umewasilishwa kwa msikilizaji bila kumwaibisha au kumuudhi.

Kulingana na Coyle (1984), tamthilia kama sanaa hupitisha ujumbe kwa hadhira yake kupitia mawasiliano baina ya wahusika mbalimbali. Kabla ya mwambao wa Pwani ya Africa Mashariki kuingiliwa na athari za kigeni zilizotoka ng'ambo, fasihi ya Kiswahili kama fasihi nyinginezo za kiafrika, ilikuwa ni ya kusimuliwa tu na ilikuwa na tanzu kama vile ngano, sanaa za maonyesho, vitendawili na methali. Utanzu wa tamthilia haukuwa na taswira kama inayo sasa, bali palikuwa na maigizo ambayo yalitolewa mbele ya hadhira kwa minajili ya kuelimisha, kuonya, kuburudisha na kufundisha maadili mema.

Anadai kuwa, maonyesho haya yalianza kubadilika baada ya maajilio ya wageni ambao walikuwa ni waarabu na wakoloni. Maonyesho haya yaliingizwa katika maandishi na kuiga mikondo ya kimagharibi ili kuchukua mkondo wa tamthilia kwa jumla. Kihistoria, tamthilia ilianza kwa kutongoa maudhui ya kidini ambayo mara nyingi yalikuwa ni uteuzi wa visa fulani kutoka katika Bibilia Takatifu ili kutoa funzo fulani. Hali hii ilibadilika hadi kuingia katika tamthilia zilizozingatia maudhui mengine kama vile tanzia na vichekesho. Katika karne ya kumi na sita hata hivyo msisitizo ulitoka katika dini na kuingiza masuala ya kijamii, hivyo tamthiliya zikaanza kuzingatia maadili ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Katika kipindi cha uhuru, Coyle (1984), anadai kuwa kabla ya miaka ya (1970), tamthilia za Kiswahili zilikuwa chache sana na nyingi kati ya chache hizo zilikuwa ni tamthilia tafsiri, kwa mfano Mfalme Edipode, Mabepari wa Venise, Julias Kaizari na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Tamthilia hizi zilitungwa kwa kufuata kanuni za Ki-Aristotle na zilikuwa katika mtindo wa kishairi, na nyingine zilitungwa katika hali ya mazungumzo.

Kulingana na yeye tamthilia andishi ya Kiswahili ilishika kasi wakati Ebrahim Hussein na Penina Muhando walipoongoza uandishi wa tamthilia ya Kiswahili. Tamthilia za kipindi hiki zilikuwa zikizungumzia masuala kama vile migongano ya kitamaduni, matatizo ya kijamii, ujenzi wa jamii mpya, uchawi na uganga.

Anaendelea kusema kuwa, utanzu wa tamthilia ndio mchanga zaidi ukilinganishwa na tanzu nyingine za fasihi ya Kiswahili. Hata hivyo chimbuko lake hasa katika mawasiliano ya moja kwa

moja baina ya msimulizi wa ngano na hadhira na majibizano baina ya msemaji na msikilizaji ni dhahiri.

Utafiti wetu ulikuwa kuhusu tamthilia na tulichunguza namna mazungumzo katika tamthilia yanavyosawiriwa na mwandishi ili kujenga na kusawiri wahusika. Tulijikita katika tamthilia kwa vile ni utanzu unaozingatia mazungumzo baina ya wahusika wawili au zaidi. Katika kufanya hivyo tulizingatia Nadharia ya Upole na namna mikakati ya upole ilivyokiukwa au kuzingatiwa ili kuendeleza maudhui. Miktadha mbalimbali ilichanganuliwa ili kutambua yale ambayo huchochea msikilizaji au mzungumzaji kukiuka au kuzingatia upole.

Mtu ana nyuso mbili; uso hasi na uso chanya. Uso hasi huwa hautaki kujitokeza. Uso hasi hutaka kuwa huru na hutaki shughuli zake kuingiliwa. Hutaka kufanya mambo bila mtu kutaka kujua anafanya nini na ni kwa nini anafanya hivyo. Uso chanya hutaka kuhifadhiwa katika mawasiliano. Msemaji anapowasiliana na msikilizaji ni lazima ahakikishe kuwa anachosema hakitamuudhi wala kumuaibisha anayezungumziwa. Msemaji anafaa kuchagua maneno yake vizuri ili ahakikishe kuwa maana iliyowasilishwa ndiyo iliyolengwa kuwasilishwa na mzungumzaji kwa msikilizaji.

Wakati wa mazungumzo, msemaji na msikilizaji wanapowasiliana ni sharti waweze kuhifadhi nyuso zao. Wataweza kufanya hivyo ikiwa watazingatia mikakati ya upole ili kuzuia kupujuana nyuso. Watazingatia mikakati ya kuwa kwenye rekodi, kuwa ndani ya rekodi, mkakati wa upole chanya na upole hasi.

Ili kuafikia haya, tulinuia kuchunguza iwapo kanuni za upole zimekiukwa au na kuzingatiwa katika *Mstahiki Meya* ya Timothy Arege. Tamthilia hii ni ya kijamii na inaweka wazi maovu ambayo viongozi huwatendea wananchi waliowachagua. Mwandishi analenga kuonyesha uhalisia kuwa maovu mengi yanayopatikana katika jamii huendelezwa na viongozi wetu tuliowaachaguaa. Tulijikita katika kuchunguza namna mwandishi huyu alitumia tamathali za usemi kama vile; methali, tashbihi, maswali balagha na sitiari. Tulichunguza ni kwa nini ametumia tamathali hizo katika mazungumzo kati ya wahusika. Matumizi ya tamathali hizi yana kusudi fulani katika kazi hii au la. Tulichunguza kusudi hizo iwapo zitakuwepo na kile alitaka kuwasilisha ili kuhifadhi uso hasi au chanya wa wahusika.

## 1.2 Tatizo la Utafiti

Katika utafiti wetu tulichunguza na kubaini namna mikakati ya upole inavyojitokeza katika *Mstahiki Meya.* Tulichunguza namna upole umekiukwa au kuzingatiwa katika kuendeleza maudhui. Tulichunguza ikiwa swala la upole lilikiukwa au lilizingatiwa kwa kutoa sababu zake. Katika kufanya hivyo tulizingatia mikakati ya upole kama walivyopendekeza Brown na Levinson (1987) na namna walivyosawiriwa. Kwa hivyo pengo tulilotaka kuziba katika Kiswahili ni kuchunguza namna nadharia ya semantiki na pragmatiki inavyoweza kutumiwa kuhakiki kazi ya fasihi.

Utafiti uliofanywa kuhusu tamthilia hii hazijashughulikia suala la upole. Hali hii ndiyo iliyotufanya kutaka kuchunguza namna mikakati ya upole ilivyodhihirika katika tamthilia hii. Mikakati ya upole inapojitokeza, je, matokeo yake ni yapi? Mikakati hii ya upole imesaidia vipi kuendeleza maudhui? Je, wasomi watakuwa na yapi ya kusema kuhusu mwandishi na kazi yake? Ni kutokana na maswali haya ndiposa tukaweza kuibuka na utafiti huu wa kuchunguza ikiwa nadharia ya upole inaweza kutumiwa kuchambua kazi ya fasihi.

Tuliweza pia kujibu ni kwa nini mikakati ya upole ilijitokeza katika kazi ya T. Arege. Tunanuia kuchunguza jinsi mikakati hii ya upole ilivyovunjwa na katika miktadha ipi. Aidha tutachunguza namna mwandishi alivyotumia tamathali mbalimbali za usemi ili kukuza maudhui.

## 1.3 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni;

(i) Kuchunguza jinsi tamathali za usemi zinavyotumika kukiuka au kudhihirisha upole.

(ii) Kuchunguza jinsi upole unavyodhihirika ili kukuza maudhui katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

(iii) Kuchunguza ni mambo gani yanayochochea ukiukaji wa kanuni za upole.

### 1.4 Maswali ya Utafiti

Je,

(i) Tamathali za usemi zinatumiwa kukiuka au kudhihirisha upole?

(ii) Mikakati ya upole imesaidia kuendeleza maudhui katika tamthilia ya *Mstahiki Meya?*

(iii) Upole katika mawasiliano huchochewa na muktadha wa mawasiliano?

### 1.5 Sababu za Kuchagua Mada

Tamthilia ni sanaa ambayo huwasilisha mchezo wa kuigiza kwa njia ya maandishi na mara nyingine kuigizwa mbele ya hadhira hai. Mwandishi yeyote ule anapotaka kuandika kazi fulani ya fasihi huwa ni wajibu wake kuteua lugha apendavyo ili kuwasilisha ujumbe wake kwa hadhira. Timothy Arege ni mwandishi wa kisasa na anayezungumzia masuala ibuka yanayoathiri jamii ya kisasa kama vile; ufisadi, udikteta, umaskini, ubinafsi, uongozi mbaya, ubadhirifu wa mali ya umma na hata ubaguzi kwa misingi ya kitabaka. Aidha mwandishi huyu anatumia lugha fulani teule ili kuwasilisha ujumbe wake.

Katika utafiti huu tuliangazia tamthilia ya *Mstahiki Meya* tuliyoteua. Kama wachanganuzi tulionelea ni vyema kuichanganua kazi hii na kuziba pengo hili katika nyanja ya usomi ili kuimarisha kazi za fasihi. Tuliichanganua kwa misingi ya nadharia ya upole ambapo tulifafanua namna tamathali za usemi zinavyotumiwa kukiuka au kudhihirisha upole ili kukuza maudhui katika tamthilia hii na namna upole unavyojitokeza miongoni mwa wahusika ili kukuza maudhui. Vile vile tulichunguza iwapo upole katika mawasiliano huchochewa na hali ya kawaida au muktadha wa mawasiliano.

Aidha matokeo ya uchanganuzi wetu yatawawezesha watafiti wa baadaye kuhakiki kazi zingine zenye mwelekeo huu aidha iwe ni riwaya au hadithi fupi na hata tanzu za fasihi simulizi kama vile; methali, semi na vitendawili. Katika kuihakiki kazi hii ni matumaini yetu kuwa utafiti wetu ulirahisisha uelewa wa ujumbe wa msanii wa kazi tuliyoihakiki kwa wasomaji watakaosoma kazi hii kwa kutaka kujiburudisha tu, bali wataelimika na kuelewa mambo mengi ambayo hawangeyaelewa barabara kabla ya kuisoma.

### 1.6 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulijikita katika kuchunguza mikakati ya upole katika *Mstahiki Meya* (2009) kwa kutumia nadharia ya upole kwa kuzingatia mtazamo wa Brown na Levinson (1987). Utafiti huu ulichunguza mikakati ya upole kama vile; mikakati ya ndani ya rekodi, mikakati ya nje ya rekodi, mikakati ya upole chanya, mikakati ya upole hasi na mkakati wa kutotekeleza kitendo kinachotishia uso.

Tulichunguza jinsi mwandishi alitumia tamathali za usemi katika mawasiliano ya wahusika wote na pia katika maelezo yake. Tulichunguza hasa kama katika tamthilia hii mikakati ya upole ilizingatiwa au la ili kukuza maudhui. Tulichunguza ukiukaji huo unatokana na sababu zipi kama huchochewa na muktadha wa mawasiliano au hali ya kawaida, na ni vipi ukiushi huu ulisaidia kuboresha kazi nzima.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Katika sehemu hii, tulijadili yaliyoandikwa kuhusu nadharia ya upole na jinsi inavyojitokeza katika kazi mbalimbali. Kazi zilizoandikwa kuhusu tamthilia ya *Mstahiki Meya* pia zitaangaziwa. Kazi zilizoandikwa kuhusu mawasiliano na matumizi ya lugha zitakuwa muhimu katika kutuongoza kufanya utafiti huu.

#### 1.7.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Nadharia ya Upole

Swala la upole limeshughulikiwa na Habwe (2010). Katika kazi hiyo anasema kuwa jamii ya waafrika hupendelea matumizi ya upole wakati wa mawasiliano. Anasema kuwa upole husaidia kudumisha heshima kati ya watu wa vyeo mbalimbali katika jamii. Habwe anasisitiza kuwa lugha inayotumiwa na wakazi wa Nairobi hudumisha upole kinyume na inavyoaminiwa kuwa mikakati ya upole haizingatiwi na wakazi hao. Anasema, kwa mujibu wa waasisi wa nadharia ya upole hasa Leech (1983); na Brown na Levinson (1978, 1987) upole ni namna ya kuokoa uso wa msikilizaji, ni utambuzi ambao mtu humwonyesha mtu mwingine kupitia kuepuka kaida au desturi fulani za mazungumzo. Habwe anaendelea kusema kuwa swala la upole ni swala lenye utata kwa sababu linahusu matumizi ya mikakati mbalimbali. Moja ya mikakati hiyo ni umri. Kwa mfano katika jamii ya waislamu ni watoto ambao husalimia wakubwa wao kwa kuwapa shikamoo. Mtoto akimpita mtu mzima bila kumpa shikamoo hiyo katika jamii ya waislamu ni ukiukaji wa kanuni ya upole. Jamii nyingi za waafrika pia hutarajia mtoto awaamkue na sio wao

waanze salamu. Iwapo mazungumzo yataendelea, mtoto hafai kukatiza mazungumzo ya mkubwa wake na akifanya hivyo basi amekiuka kanuni za upole. Uchunguzi wa Habwe unaonyesha kuwa matumizi ya maneno kama tafadhali, pole, samahani hutumika sana katika mazungumzo ya watu wa Nairobi. Matumizi ya maneno haya kwa kawaida huleta uhusiano mwema na upole huwa dhahiri.

Katika kazi hii, Habwe alikuwa anachunguza mikakati ya upole ambayo hutumiwa na watu wa Nairobi. Mikakati mingine inayotumiwa si ya moja kwa moja. Msemaji anawaza kutumia maswali badala ya kusema jambo moja kwa moja. Msemaji pia anaweza kutumia mkakati wa kujitweza ili kumfurahisha msikilizaji, kwa mfano,

1. “Ningekuwa dereva mzuri kama wewe ningefurahia sana.”

Habwe anasema kuwa matumizi ya mikakati ya upole kati ya wakazi wa Nairobi husaidia kuhifadhi uso wa msikilizaji. Watu wa Nairobi hujaribu kutumia mikakati ya upole wanapowasiliana katika hali ya kawaida. Utafiti huu wa Habwe utatusaidia kwa vile katika kazi yetu, tutachunguza mikakati ya upole iliyokiukwa au iliyozingatiwa na mwandishi T. Arege ili kuendeleza maudhui katika tamthilia ya Mstahiki Meya.

Habwe (2010), ameshughulikia pia swala la upole akizingatia kanunu za upole za Grice, ambazo ni; kanuni ya uhusiano, kanuni ya ubora au ukweli, kanuni ya namna au jinsi na kanuni ya kiasi. Grice (1975), alipendekeza kanuni nne za upole. Katika kazi hii ya Habwe amezingatia kanuni hizo za Grice (1975) na (1977) na alichunguza jinsi wanasiasa wa Mombasa na Nairobi wanavyotumia mikakati ya upole wanapohutubia umati wa watu. Ili kuweza kuwashawishi wapiga kura wanasiasa hutumia mikakati mbalimbali ili wawashawishi wananchi kuwapigia kura. Katika kazi hii, Habwe alichunguza mikakati ya upole ambayo wanasiasa wa Nairobi na Mombasa hutumia ili kupata kura kutoka kwa wananchi. Mchango wa utafiti huu kwa utafiti wa sasa ni kwamba,tutaweza kutumia mikakati iyo hiyo ya upole ambayo ni;mikakati ya upole chanya,mikakati ya upole hasi, mikakati ya ndani ya rekodi na mikakati ya nje ya rekodi kuchanganua kazi ya fasihi. Tutachunguza namna mwandishi alivyotumia mikakati hii yote ya upole katika kuiboresha kazi yake. Mchango wake ulikuwa wa manufaa sana katika utafiti wetu.

Raitania (2014) katika tasnifu yake, alichunguza mikakati ya upole katika vipindi vya runinga na hasa mawaidha na Bi Mswafari katika runinga ya Citizen. Kipindi hiki hupeperushwa na runinga ya Citizen kikiwa ni kipindi cha kutoa mawaidha kuhusu ndoa. Alieleza jinsi Bi Mswafari na watangazaji Kanze Dena na Lulu Hassan huendeleza kipindi hiki. Anaeleza jinsi mikakati ya upole imezingatiwa katika kipindi hiki, hivi kwamba wakati wa mazungumzo watangazaji hawa huhakikisha kuwa wamewasiliana kwa njia iliyo bora ili kuhifadhi nyuso za wasikilizaji au watazamaji. Kazi hii pia itakuwa ya manufaa kwetu kwa vile tutajikita katika mikakati iyo hiyo ya upole tukichunguza namna ilivyokiukwa au kuzingatiwa na ni kwa sababu gani. Aidha tutachunguza mambo yanayochochea ukiukaji au udhihirishaji wa kanuni za upole.

Walubengo, (2010) alishughulikia swala la upole katika nyimbo za sherehe za jando za jamii ya wabukusu kwa kutumia mtazamo wa nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1978) hasa kipengele cha mikakati ya kuokoa uso. Utafiti wake utakuwa wa manufaa kwetu kwa vile ni mikakati iyo hiyo ya upole tutakayotumia kuchanganua kazi ya fasihi andishi ambayo ni tamthilia. Tutajikita katika kuchanganua mikakati ya kuokoa uso wakati wa mawasiliano kati ya msemaji na msikilizaji.

Owino (2011) alishughulikia uchanganuzi wa matini teule wa nyimbo za Fousine Munishi akitumia mtazamo wa nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987) hasa kipengele cha kuokoa uso. Kazi hii itakuwa ya manufaa kwetu kwa kuwa kutachanganua tamthilia ya *Mstahik*i *Meya* kwa mihimili ya nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987).

Mjomba (2012) alishughulikia suala la upole katika nyimbo za harusi kutoka jamii ya wadawida akitumia mtazamo wa nadharia ya upole ya Brown na Levinson (1987). Utafiti wake vile vile utakuwa wa manufaa kwetu.

Hakuna kazi yeyote iliyoandikwa kuzungumzia jinsi upole umekiukwa au na kuzingatiwa katika *Mstahiki Meya* ya T. Arege.  Hata hivyo kazi zilizofanywa kuhusu mawasiliano na matumizi ya lugha zitasaidia katika utafiti huu. Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa matumizi ya lugha hudhihirika katika muktadha maalum wa jamii na kuwa wakati wa mawasiliano ni muhimu kuzingatia muktadha. Katika kazi yetu tumechunguza ni vipi muktadha wa mawasiliano unaweza

kuchochea matumizi ya lugha bila kuzingatia upole, hivyo maoni yao ni muhimu katika kazi yetu.

Kazi zilizoandikwa na watafiti wengine zimefanyiwa udurusu hasa zinazohusu matumizi ya lugha kwa njia tofauti tofauti na kubainika kuwa hakuna kazi maalum iliyoandikwa swala la upole katika *Mstahiki Meya* ya Timothy Arege.

Lackoff (1976) anahusisha lugha na vitengo vingine vya jamii kama ilivyo sayansi na kudai kuwa pekee haiwezi kujitosheleza. Mtaalamu huyu anadai kuwa utafiti wowote wa kiisimu lazima ujikite katika kueleza sababu za watu kuongea jinsi wafanyavyo. Anadai kuwa maswala mengi katika lugha kama vile muktadha, sababu ya tamko au usomi fulani, jinsi ya kutafsiri usemi, upole katika usemi ni baadhi ya mambo ambayo hayashughulikiwa kikamilifu.

Kulingana na Lackoff (1976), sio sawa kuzingatia sintaksia pekee katika matini na kupuuza muundo ndani ya tungo. Ni muhumu kujiuliza ni kwa nini mzungumzaji anazungumza jinsi afanyavyo. Anatoa kauli kuwa si sawa kuwa na uamuzi wa jumla kwamba kila binadamu mwenye akili razini lazima atumie njia fupi anapozungumza. Anasisitiza kuwa ukamilifu wa maana hutegema alichokusudia msemaji. Hata kama anakubali kuwa si sawa kuwa na uamuzi wa jumla anakubaliana na kanuni za upole za Grice (1975) ambayo ni:

(i) Ufaafu wa kinachosemwa kwa anayesikiliza yaani uhusiano.

(ii) Thamani na ukweli wa kinachosemwa.

(iii) Kiasi cha yanayosemwa

(iv) Namna au jinsi ya kusema.

Kazi hii itachangia pakubwa katika utafiti wetu kwa sababu baadhi ya mambo tutakayochunguza ni matumizi ya lugha kwa kuzingatia kanuni nne za mawasiliano za Grice (1975).

Wakati wa mawasiliano msemaji na msikilizaji lazima waseme mambo ambayo yana uhusiano na yale ambayo wanazungumzia. Kwa mfano, iwapo anazungumza kuhusu magonjwa fulani, ni sharti mazungumzo yao yasalie kuwa kuhusu ugonjwa na wala wasilete mada ambayo haihusiani na magonjwa kama masuala ya mavazi au hata magari.

Msemaji na msikilizaji wanapowasiliana ujumbe wao ni sharti uwe wa kweli hivi kwamba wanaweza kudhibitisha kile wanachosema. Waseme mambo yaliyo ya kweli kiasi kwamba wanaweza kudhibitisha ukweli wa kile wanachosema. Kwa mfano, wananchi wa mji wa Cheneo wanapolalamika kuwa hakuna dawa hospitalini wanadhibitisha hali hii kwa kutoa idhibati kuwa watu wanafa kwa ajili ya ukosefu wa dawa hospitalini. Wakaazi wa cheneo basi, wamezingatia kanuni ya Grice (1975) ya kusema mambo yaliyo ya kweli.

Msemaji na msikilizaji wanapowasiliana ni vyema watumie maneno machache na sio kutumia maneno mengi ambayo hayana faida kwao. Kwa mfano, Meya Sosi anapomwambia Siki kuwa wanacheneo ndio waliomchagua na watamchagua kwa mara nyingine anamaana kuwa wanafurahia uongozi wake na kwamba yale Siki anamweleza kuhusu uongozi wake mbaya si ya muhimu kwake.

Aidha namna au jinsi ya kuwasilisha ujumbe ni muhimu kwa msikilizaji na mzungumzaji. Ni muhimu msikilizaji na msemaji kuzingatia namna ambayo watawasiliana ndiposa wasipujuane nyuso zao. Kwa mfano, unapotaka kumnyima mtu kuna namna utamwambia ndiposa asiadhirike kama vile kuomba msamaha.

Trudgil (1983) anasema kuwa kila jamii ina sheria zinazoongoza matumizi ya lugha, mwingiliano na mtagusano wa wanajamii. Anasema kuwa katika mawasiliano, ni lazima mtu aelewe utamaduni wa jamii yake ili aweze kutumia lugha inavyotarajiwa. Ni muhimu kuelewa ni vipi mtoto anafaa kuongea na wakubwa wake ili asionekane kukiuka matarajio ya jamii kuhusu namna ya kuzungumza. Mtoto anatarajiwa kuongea kwa heshima akizungumza na mkubwa wake kinyume na afanyavyo akiwa na watoto wenzake. Iwapo mtoto atazungumza na mtu mkubwa bila kuzingatia heshima basi atakuwa amekiuka kanuni ya namna.

Guiner (1998) anaeleza namna lugha ilivyotumiwa kumdhalilisha lakini hakufa moyo. Anaeleza kuwa alidhalilishwa na wanaume waliokuwa na taasubi ya kiume alipokuwa akisomea uanasheria. Wanaume walikuwa wakitumia lugha inayokiuka kanuni za upole kwa sababu hawakuthamini wanawake. Kazi hii vile vile itasaidia katika kuchunguza na kuelewa ni kwa nini wahusika wengine katika *Mstahiki Meya* kama vile Meya Sosi walitumia lugha bila kuzingatia

upole. Guiner anathibitisha kwamba, dharau linaweza kumfanya mtu kumzungumzia mwingine bila kuzingatia upole.

Guiner (1998) anasema kuwa hata kama alidunishwa kwa kuwa mwanamke alionyesha upole hata alipokuwa na tajriba kubwa kuhusu jambo. Kwa kuwa kazi yetu inahusu swala la upole na namna mhusika anaweza kukiuka mikakati ya upole, tutachunguza udunishaji wa Mhusika Mkuu; Meya Sosi kama ni baadhi ya vichocheo vya ukiukaji wa kanuni za upole katika *Mstahiki Meya.*

Kupitia udurusu uliofanywa na marejeleo ya vitabu vilivyosomwa, ni dhahiri kuwa suala la upole katika mawasiliano halijatafitiwa katika tamthilia hii.

Kulingana na Wamitila (2003) lugha ni chombo muhimu katika mawasiliano. Msemaji au mwandishi anaweza kuathiri mawasiliano iwapo atatumia lugha vibaya. Anasisitiza kuwa matumizi ya lugha ni kipengele muhimu cha kuchanganua jamii inayohusika. Kauli hii ni muhimu katika utafiti wetu kwa sababu tutajaribu kuchunguza ni nini kilichomchochea Timothy Arege kutumia lugha inayokiuka au inayozingatia kanuni na mikakati ya upole.

### 1.7.2 Yaliyoandikwa Kuhusu Tamthilia ya Mstahiki Meya

Tamthilia ya *Mstahiki Meya* (2009) imeshughulikiwa na wahakiki mbalimbali. Biasha (2015) alishughulikia uhakiki wa usimulizi katika tamthilia hii kwa kutumia nadharia ya naratolojia kwa mtazamo wa Genette (1972-1983). Alilenga kubainisha vipengele vya usimulizi na kujadili dhima ya vipengele hivyo katika Tamthilia hiyo. Utafiti wake hautakuwa wa manufaa kwetu kwa kuwa tutajikita katika kuchanganua tamthilia hii kwa msingi wa nadharia ya upole ambayo ni nadharia ya semantiki.

Ndege (2013) amechunguza ukuaji wa muundo na mawazo katika tamthilia za T. Arege ikiwemo *Mstahiki Meya*. Ameshughulikia mchango wa matumizi ya lugha katika kazi hizo. Pia mchango wa wahusika katika kuendeleza dhamira na maudhui. Utafiti wake ulitufaa wakati wa kuchunguza kipengele cha tamathali za usemi, ingawaje utafiti huu umejifunga na usawiri wa wahusika, wakati na daraja na sauti za usimulizi katika *Mstahiki Meya*.

Okwena (2013) amechunguza matumizi ya jazanda katika tamthilia tatu za T. Arege.Tamthilia hizi ni pamoja na *Chamchela, Kijiba Cha Moyo* na *Mstahiki Meya*. Utafiti huu umeshughulikia usimulizi katika tamthilia hizo kwa kutumia nadharia ya naratolojia. Utafiti huu utatufaa kwa vile tunanuia kuchunguza namna tamathali za usemi zinavotumiwa kukiuka au kudhihirisha upole.

Hata hivyo tahakiki nyingi ambazo zinapatikana kuhusu tamthilia hii ni miongozo ambayo imenuia kuwasaidia walimu na wanafunzi wa shule za upili kuielewa tamthilia hii ambayo inatahiniwa kwa hivi sasa katika mtihani wa Kiswahili wa kitaifa wa kidato cha nne. Baadhi ya walioandika miongozo kuhusu Tamthilia ya *Mstahiki Meya* ni pamoja na Mbuthia (2012), Kaui (2012), Mbuvi na Were (2012), King'ei, Kyalo na Mwangi (2012), Omboga (2012), Ryanga na Maina (2012) na Muturi (2012). Waandishi hawa wamehakiki tamthilia hii kwa kuzingatia vipengele vya msuko, maudhui, wahusika na matumizi ya lugha. Kwa hivyo, katika tahakiki zao, hawakushughulikia kipengele cha upole. Utafiti wetu umeshughulikia mikakati ya upole katika tamthilia iyo hiyo kwa kutumia nadharia ya upole. Utafiti wao umetoa mchango maalum na nyongeza kwa yale ambayo yamesemwa na wahakiki waliotutangulia.

### 1.8 Msingi wa Kinadharia

Tutachanganua kazi hii kwa kutumia nadharia ya upole. Upole ni dhana inayorejelea hali ya kuwa mtaratibu wakati wa mazungumzo. Nadharia ya upole iliasisiwa na Brown na Levinson (1987). Nadharia hii ya upole inadai kuwa mtu hutumia mikakati mbalimbali ili kuhifadhi uso wa msikilizaji. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), kuna aina mbili za uso; Uso chanya na Uso hasi. Uso chanya hutaka kuhifadhiwa na kutambuliwa. Hii inamaanisha kuwa unapoongea na mtu, unafaa ujaribu usimuaibishe wala kumuudhi. Uso huu ni ule mtu anapenda kusifiwa au kushirikishwa katika shughuli za kijamii yaani, kutobaguliwa panapokuwa na mazungumzo ya familia au hata mikutano. Binadamu yeyote ule anapokosa kutambuliwa kwenye mazungumzo au shughuli inayohusiana hasa na familia yake huwa anaona kubaguliwa au kudharauliwa hivyo basi hudhuriwa ikiwa mzungumzaji au msikilizaji hatajali maslahi ya yule anayewasiliana naye.

Katika mazungumzo yoyote lazima kuwe na kuelewana kati ya mzungumzaji na msikilizaji ikiwa mawasiliano yatafikia kilele cha yaliyolenga. Kufanikisha mazungumzo haya lazima kuwe

na lugha ya heshima na upole kwa wahusika wakiwa na lengo la kutomdharau yeyote au kupujuana uso. Ni kutokana na kutaka kuheshimiana ndipo dhana ya upole ilizuka ili kuhifadhi uso chanya wa mzungumzaji au msikilizaji

Uso hasi huwa hautaki kuingiliwa. Mawazo na maoni yake huwa ni mwisho na ukijaribu kupinga au kurekebisha unamuudhi. Kwa mfano, iwapo mzazi atajiingiza katika mambo ya mtoto wake bila idhini, basi mtoto ataona kuwa amenyimwa haki ya kujiamulia mambo vile anavyotaka. Uso hasi hutishiwa wakati mtu hawezi kujinasua katika masuala ya wazazi, walimu au hata watu waliotuzidi umri. Tendo hili huenda likamdhuru mzungumzaji au hata msikilizaji na kumfanya mmoja wao kuomba msamaha. Uso hasi basi ni uhitaji wa kutaka kusalia huru ndio mzungumzaji atakuwa mwepesi wa kumtafuta msikilizaji.

Kulingana na wataalamu hawa, iwapo kuna uwezekano wa kuathiri hisia za mtu ni lazima mtu atumie mikakati ifaayo katika mawasiliano. Mikakati atakayotumia itategemea uhusiano uliopo baina ya msemaji na msikilizaji. Nadharia hii inatambua mikakati minne ambayo mtu anaweza kutumia katika mawasiliano ambayo ni:

(i) Mikakati ya ndani ya rekodi

(ii) Mikakati ya nje ya rekodi

(iii) Mikakati ya upole chanya

(iv) Mikakati ya upole hasi

Mikakati ya ndani ya rekodi hutumiwa wakati watu ambao wamezoeana wanazungumza. Watu hawa ni kama vile watu wa familia, marafiki au watu wanaofanya kazi pamoja na wana urafiki wa karibu. Unapotumia MDR huwa hujihadhari sana kuhifadhi uso wa msikilizaji. Mikakati hii hutumiwa na watu ambao hutaniana. Ni mkakati unaotumia njia ya upole kurekebisha tabia ya mtu fulani au kusema jambo kwa kujaribu kupunguza tishio la uso wa msikilizaji.

Nadharia ya J.L. Austine (1975) ya kitendo usemi imesema kwamba ili kuwe na maelewano kati ya msikilizaji na mzungumzaji, lazima watu wafuate kanuni nne za mawasiliano. Moja kati ya hizo ni kusema ukweli. Ndiposa waswahili husema, sema kweli japo ni uchungu. Hivyo mkakati

huu husema ukweli kwa njia ya moja kwa moja ijapo upole hutumika; vile vile hupunguza athari kubwa kwa msikilizaji, kwa mfano;

2. Ungekuwa na pesa kweli, ungetupeleka hoteli ya “680”.

3. Umeshindwa kutunza mume wako watamani wa wenzio, ukiona vyaelea jua vimeundwa.

Mazungumzo haya huendelezwa na watu wanaotaniana sana au familia zenye ushirikiano wa karibu. Njia hii hutumiwa kurekebisia tabia zinazokera katika jamii zetu. Vile vile mkakati huu unaweza kutumiwa kumwingilia bwana au bibi arusi iwapo atagunduliwa kuwa ana kasoro fulani.

Mikakati ya nje ya rekodi hutumika pale ambapo msemaji anataka jambo lifanywe lakini hasemi moja kwa moja. Huu ni mkakati unaotumia mafumbo au njia ya mzunguko kuelezea jambo fulani. Katika mazungumzo hayo msikilizaji au hadhira huwa si rahisi kumuelewa mzungumzaji anacholenga ni kitu gani au ana maana gani. Hata hivyo, mzungumzaji au msikilizaji anayetumia njia hii huwa anafahamiana au anaingiliana sana na hadhira. Mzungumzaji huteua maneno ambayo hayatoi ujumbe kwa njia ya moja kwa moja bali kwa mafumbo na hadhira ikaelewa ujumbe huo bila utata wowote.

Mikakati ya upole chanya hutumika pale ambapo msemaji na msikilizaji wanajuana kiasi. Huwa msikilizaji na msemaji wanajuana lakini msemaji huwa makini asiudhuru au kuaibisha uso wake. Huwa msemaji anajaribu kutambua cheo na nafasi ya msikilizaji katika jamii. Kwa mfano iwapo unataka kununua bidhaa fulani na huna pesa unaweza kumwomba pesa bila kutatizika sana. Mkakati huu hutumiwa kuhifadhi hadhi ya mzungumzaji au na msikilizaji. Hadhi yake yaweza kuhifadhiwa kwa kumfanya ajihisi kwamba anatambuliwa na jamii anayoishi nayo au kama ni kwenye mkutano anashirikishwa vilivyo katika masuala yanayozungumziwa.

Kumhusisha vilivyo na kumheshimu kutapunguza migogoro au taharuki ambayo ingezuka miongoni mwa hadhira husika kwa sababu ya tashwishi zitakazoibuka. Kwa mfano,

4. Lo! Maria, chai hii ni tamu sana. Umechemsha ikachemka.
Naomba sukari kidogo niongezee.

Japo mzungumzaji anataka kumjulisha Maria kwamba chai aliyopika ina upungufu wa sukari, ameanza kumsifu kwanza alafu akaomba sukari. Hii ni njia mojawapo ya kutambua upishi mzuri wa Maria ingawaje una kasoro fulani. Mzungumzaji anapotumia maneno kwa njia hii, atakuwa anaendeleza mkakati wa upole chanya kwa njia stadi ili kukwepa kumuathiri msikilizaji.

Mikakati ya upole hasi hutumika pale ambapo msemaji anajihisi kuwa anamsumbua msikilizaji. Unapotaka kuelewa njia na mtu ambaye hamjuani itabidi umtahadharishe kwanza kuwa ungetaka kuongea naye kwa mfano.

5. “Samahani unaweza kunielekeza njia ya kwenda Kayole”.

Mzungumzaji au msikilizaji hujaribu kutumia mbinu tofauti tofauti ili kuhifadhi uso hasi wa hadhira yake. Kwa mfano, anaweza kutumia njia ya maswali mengi ili kupata jibu la jambo analotaka kutoka kwa mzungumzaji, au msikilizaji. Njia hii huwa ndefu au ya mzunguko na yenye kutumia wakati mwingi ilimradi jibu lipatikane. Pia mzungumzaji anaweza kutumia njia za uwongo au kumdanganya msikilizaji kwa dhamira ya kuepuka kudhuru uso wake. Kwa mfano, mzungumzaji anapomwuliza msikilizaji swali kama:

6. Waonaje viatu vyangu, je, vinapendeza?

Japo viatu vyenyewe havipendezi, itamwia vigumu msikilizaji kumwambia ukweli kwa sababu ya kuogopa kumpujua uso wake, badala yaje atamsifu na hata kumwuliza alikonunua.

(Brown na Levinson 1987:66) wanasema kuwa dhana ya uso ilitokana na kazi ya (Goffman 1959). Goffman ndiye aliyekuwa mwasisi wa dhana ya uso ambayo ilikuwa ndiyo msingi wa nadharia ya upole. Dhana ya uso ilitokea Uchina ambapo aliikopa na kuitumia kuashiria hali ya mzungumzaji na msikilizaji wakiwa wanawasiliana wafanye hivyo bila kuathiriana na kupujana nyuso.


Goffman anaendelea kusema kwamba uso kama kifaa muhimu cha kijamii,mtu hukipata wakati wa mtagusano maalumu katika jamii. Ndiposa anasema kuwa binadamu ana uso wa hadhira na uso usiokuwa wa hadhira. Jambo hili linamaanisha kuwa binadamu yeyote ule huwa na aina mbili za uso. Kwa hivyo uso ambao ni ishara bayana katika jamii ni sharti kuthaminiwa. Ni

kutokana na nadharia ya uso ambapo nadharia ya upole ilizuka ili iokoe uso kutokana na matendo ya kuutishia ambapo husababishwa na mitagusano ya kijamii.

Kuwepo kwa tishio la uso wa mtu hujulikana kama tendo la kutishia uso. Ili kuwa na maelewano kati ya kundi au watu fulani wanaowasiliana, lazima lugha inayotumika iwe na maneno ya heshima yenye kuonyesha upole na ishara zenye kuelekeza vyema.

Mawasiliano yanayopitishwa kwa kutumia maneno machafu au yasiyokuwa na adabu huchangia tendo la kutishia uso. Kwa sababu hii msikilizaji au mzungumzaji lazima aweze kuteua maneno atakayotumia kuwasilisha ujumbe wake ili kufikia lengo la kuwasiliana bila kupujua nyuso za hadhira lengwa. Maelezo ya watalaamu hawa yanaweza kudhihirishwa kupitia kwa kielelezo kifuatacho.

Kielelezo 1: Vitishio vya uso




Lackoff na Johnson (1980) wakichangia kuhusu dhana ya uso wanadai kuwa "uso" ni sitiari ambayo hutumika kila wakati. Wanadai kuwa kila wakati katika mazungumzo ni lazima kukumbuka kuwa mtu ni lazima ajaribu asimuudhi, kumuaibisha au kutotambua nafasi ya mtu katika jamii. Jambo hili ni la kweli kwani hakuna wakati mtu huwa na nia ya kuudhi mwenzake katika mazungumzo ya kawaida. Dhana ya uso inaweza kutokuwa na maana pale ambapo watu wanateta au hawaheshimiani hata kidogo. Watu wanapoteta huongozwa na hisia za hasira na hivyo huwa vigumu kuzingatia upole.

Mtalamu mwingine ambaye alishughulikia mawasiliano na dhana ya upole ni (Grice 1975). Kulingana na Grice (1975) mawasiliano hukamilika kutokana na juhudi za msikilizaji na msemaji. Wote wawili wana jukumu la kuhakikisha ya kwamba mawasiliano yameendelezwa kwa njia ifaayo. Katika kazi yake anasisitiza kwamba lazima pawe na makubaliano katika mawasiliano yoyote.

Katika kazi yake Grice alitoa kanuni nne ambazo ni muhimu katika mawasiliano. Kanuni hizi alizitaja kama;

(i) Kanuni ya ukweli au ubora

(ii) Kanuni ya uhusiano

(iii) Kanuni ya kiasi

(iv) Kanuni ya namna au jinsi.

Kanuni ya ubora inasema kuwa katika mawasiliano sema jambo ambalo unajua ni ukweli kiasi kwamba unaweza kudhibitisha na kutoa ushahidi. Habari zitakazotolewa na msemaji ni sharti ziwe za kweli na ambazo ana uhakika nazo.

Kanuni ya uhusiano inadai kuwa unapozungumza ujihusishe na mada inayozungumziwa. Usichanganye mambo ambayo hayahusiani na yale yanayosemwa, yaani, asiseme ambo ambayo yako nje ya mada inayozungumziwa au muktadha wa mawasiliano. Hata hivyo kanuni hii inaweza kukiukwa iwapo mtu anataka kujiepushaa na yanayozungumziwa.

Kanuni ya kiasi inadai kuwa mzungumzaji atumie maneno kwa kiasi Fulani na asiongeze maneno mengi ambayo hayaongezi maana kwa kile anachotaka kusema. Wakati mwingine mtu anaweza kuwa anasema kitu lakini kabla aseme awe amepita njia ndefu sana. Hali hii ndiyo hupelekea mtu kuambiwa "tafadhali fupisha kauli yako".

Kanuni ya namna inasema kuwa, katika mawasiliano, kinachosemwa lazima kiwe wazi. Kusiwe na hali ya kujaribu kukisia au kujaribu kuelewa msemaji anataka kusema nini. Ujumbe usiwe na utata wowote, uwe na mpangilio na utaratibu mzuri; aidha mfupi au lugha nyepesi inayoeleweka kwa urahisi na msikilizaji.

### 1.10 Mbinu za Utafiti

Katika mbinu za utafiti, tutafafanua, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji data, uchanganuzi wa data na uwasilishaji wa data.

#### 1.10.1 Uteuzi wa Sampuli

Sampuli tunayotumia ni sampuli lengwa ambayo ni tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Kwa mujibu wa (Mugenda na Mugenda 1999:50) aina hii ya sampuli hutumika katika utafiti unaokusudiwa kupata habari za kina bila kujumlisha. Kwa kurejelea haya maelezo, tulichagua Tamthilia hii kwa sababu itatusaidia kupata habari za kina za suala tunalochunguza la Upole.

#### 1.10.2 Ukusanyaji wa Data

Katika ukusanyaji wa data, kwanza kabisa tutaisoma Tamthilia tuliyoiteua ambayo ni Mstahiki Meya na kuchunguza tamathali za usemi zilizotumiwa na mwandishi ili kukuza maudhui na kuendeleza dhamira. Tutazichuja tamathali hizo ili tusalie na zile hasa zitakazotumika kuonyesha udhihirishaji wa upole katika tamthilia. Aidha tutachunguza mikakati ya Upole ambayo ni mikakati ya upole chanya, mikakati ya upole hasi, mikakati ya nje ya rekodi na mikakati ya ndani ya rekodi.Pia tutasoma tasnifu za wasomi wengine zilizoandikwa kuhusu nadharia ya upole na tamthilia ya *Mstahiki Meya.*

#### 1.10.3 Uchanganuzi wa Data

Data tutakayopata tutaichanganua kulingana na malengo ya utafiti wetu pamoja na mihimili ya Nadharia ya Upole. Kwa kutumia mihimili ya nadharia hii tutachanganua tamathali za usemi ambazo mwandishi kupitia kwa wahusika wakuu pamoja na wale wasaidizi wanatumia kukiuka upole. Aidha tutaweza kuchanganua iwapo tamathali za usemi hutumiwa kukiuka na kudhihirisha upole ili kukuza dhamira na kuendeleza maudhui na hutokana na hali ya kawaida au huchochewa na muktadha wa mawasiliano.

Hata hivyo, suala la upole litakuwa muhimu kuzingatiwa na waandishi ili waweze kuokoa nyuso za hadhira lengwa. Kupitia utafiti huu, wanaisimu watakuwa na msingi bora wa kutafiti zaidi tamthilia zilizosalia kutumia mtazamo mwingine ili kuendeleza na kuhifadhi fasihi andishi.

### 1.10.4 Uwasilishaji wa Data

Baada ya kukusanya na kuchanganua data, uwasilishaji wa matokeo yetu utafanywa kwa njia ya maelezo. Uwasilishaji huu utahusu maelezo ya namna tamathali za usemi zinavyotumika kukiuka mikakati ya upole ili kukuza maudhui kwa kurejelea Tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Vile vile tutaeleza iwapo upole katika mawasiliano huchochewa na hali ya kawaida au huchochowa na muktadha wa mawasiliano.

# SURA YA PILI

# MIKAKATI YA UPOLE KATIKA KUJENGA USHIRIKIANO KATIKA MAZUNGUMZO

## 2.0 Utangulizi

Ili kuweza kufafanua mikakati ya upole katika mazungumzo, ni muhimu kuelewa Nadharia ya Upole kikamilifu. Sura hii inafafanua nadharia mbalimbali za upole zilizobuniwa na waasisi mbalimbali ili kufafanua dhana ya upole. Miongoni mwa waasisi wa nadharia hii ni Grice (1975), Leech (1983) na Brown na Levinson (1987). Katika sura hii tumeangalia kanuni za ushirikiano za Grice (1975), kanuni za upole kulingana na Leech (1983) na mitazamo ya Brown na Levinson (1987).

Baada ya kufafanua nadharia hizi za upole, tutatumia nadharia ya upole ya Brown na Levinson kuchanganua tamathali za usemi zilizotumiwa kukiuka au na kudhihirisha upole.

## 2.1 Kanuni za Ushirikiano (Grice, 1975)

Grice alipendekeza kanuni nne za ushirikiano katika mazungumzo yoyote. Kanuni hizi ni; kanuni ya ukweli, kanuni ya idadi, kanuni ya uhusiano na kanuni ya namna.

### 2.1.1 Kanuni ya Ukweli

Kanuni hii inasema kuwa katika mawasiliano msemaji anafaa kusema jambo ambalo anajua ni ukweli kiasi kuwa anaweza kudhibitisha. Kwa mfano:

7. Msemaji: Una watoto wangapi?
   Msikilizaji: Wengi.

Katika mazungumzo haya msikilizaji hajatoa maelezo yake vyema kwa kuwa jibu lake "wengi" haliwezi kudhibitishwa kwa kuwa wengi inaonyesha idadi ya jumla tu. Angejibu kwa kusema idadi kamili ya watoto alionao kwa mfano wawili au watatu kwa kuwa idadi hiyo inaweza dhibitishwa.

8. Msemaji: Una watoto wangapi
Msikilizaji: Nina watoto wawili.

### 2.1.2 Kanuni ya Idadi

Kanuni hii inadai kuwa mzungumzaji anafaa kusema maneno ambayo yanahitajika tu .Asiseme maneno mengi ambayo hayana mchango wowote ule kwa yanayosemwa. Wakati mwingine mtu anaweza kuwa anasema kitu fulani lakini kabla aseme awe amesema maneno mengi sana. Kwa mfano;

9. Msemaji: Mama unaenda wapi?
Msikilizaji: Nilikua natakikana nifike kanisani kabla ya saa mbili kwa sababu ibada inaanza saa mbili na nusu.

Katika mazungumzo haya msikilizaji anafaa kutoa jibu la moja kwa moja badala ya kutumia maneno mengi kueleza kule ambako alikuwa anaelekea. Ndiposa kanuni ya idadi iwe imezingatiwa katika mazungumzo haya msikilizaji alifaa kujibu “ninaenda kanisani” Msikilizaji amekiuka matumizi ya upole katika mazungumzo haya kwa kusema maneno mengi yasiyo na maana.

10. Msemaji: Mama, unaenda wapi?
Msikilizaji: Naenda kanisani.

### 2.1.3 Kanuni ya Uhusiano

Kanuni hii inadai kuwa msemaji ajiepushe na kusema mambo ambayo yako nje ya mada. Kwa mfano;

11. Msemaji: Unaitwa nani?
Msikilizaji: Tulisoma na nduguyo katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Katika mazungumzo haya msikiliza ametoa jibu ambalo halina uhusiano na swali aliloulizwa. Msikilizaji amekiuka kanuni ya uhusiano kwa kutoa jibu lisilo na uhusiano na jina lake. Alitarajiwa kutaja jina lake kama vile; “naitwa Maria” na sio kusema namna alivyosoma na nduguye msemaji katika chuo kikuu kimoja. Kwa mfano;

12. Msemaji: Unaitwa nani?
Msikilizaji: Naitwa Maria.

Kanuni ya uhusiano inaweza kukiukwa iwapo mambo yanayosemwa hayamfurahishi msemaji au na msikilizaji. Mada inaweza kubadilishwa kimaksudi ili uso chanya wa msikilizaji au mzungumzaji usidhurike.

### 2.1.4 Kanuni ya Namna

Kanuni hii inasema kuwa msemaji anafaa kujiepusha na kauli tata ambazo zinaweza kuibua fasiri mbalimbali. Msemaji anafaa kusema anachosema kwa uwazi kiasi kwamba msikilizaji asichukue muda mwingi kufikiria kile msemaji alikusudia kusema. Aidha kusiwe na hali ya kujaribu kukisia au kujaribu kuelewa msemaji anataka kusema nini. Kwa mfano;

13. Msemaji: Upishi wako wa wali wapendeza.
    Msikilizaji: Wataka nikufunze kupika?

Katika mazungumzo haya msikilizaji atakisia iwapo msemaji alitaka afunzwe kupika wali au alitaka kupikiwa wali na anayewasiliana naye. Sababu kuu ni kwamba msemaji aliwasilisha maelezo yake kwa njia isiyo wazi kwa hivo ikabidi msikilizaji akisie kile msemaji alitaka kusema.

Kanuni za ushirikiano za Grice (1978) haziwezi kufuatwa kama sheria kwani wakati mwingine msikilizaji anaweza kuwa anataka kupewa habari kwa undani kuhusu jambo fulani. Jambo kama hili linapotokea, msemaji hukiuka kanuni ya idadi kimaksudi. Wakati mwingine kanuni ya namna pia inaweza kukiukwa wakati msemaji anataka kusema jambo kwa mtu mmoja na hataki wengine ambao wako na mtu huyo wajue kile ambacho msemaji alinuia kusema. Atafanya hivyo iwapo yale aliyokusudia kusema ni siri. Kwa kufanya hivyo, atakua amekiuka kanuni ya namna. Anaweza kusema jambo kwa njia ambayo anayelengwa ataelewa lakini waliopo ambao ujumbe si wao hawataelewa.

Ni wazi kuwa bila ushirikiano mitagusano ya watu ingekuwa jambo gumu sana na kanuni ya ushirikiano na kaida za Grice hutumika katika mitagusano ya maongezi kwa jumla. Kwa mfano, kujibu swali la maswala ya kisiasa kwa kueleza maswala ya ndoa kunavunja kanuni ya uhusiano. Kwa mfano;

14. Msemaji: Juma atawania nyadhifa ipi katika uchaguzi mkuu ujao?
    Msikilizaji: Ndoa yake imesambaratika kutokana na mzozo wa kinyumbani.

Mazungumzo haya yamevunja kanuni ya uhusiano kwa vile tulitarajia msikilizaji ataje nyadhifa atakayowania Juma katika uchaguzi wanaorejelea. Kwa mfano;

15. Msemaji: Juma atawania nyadhifa ipi katika uchaguzi mkuu ujao?
    Msikilizaji: Juma atawania ugavana.

Kwa kutaja ugavana kuna uhusiano na mambo ya kisiasa kwa sababu ugavana ni mojawapo wa nyadhifa inayowaniwa katika uchaguzi.

**2.2 Kanuni za Upole Kulingana na Leech (1983)**

Leech (1983) ni mwanaisimu aliyeangazia suala la upole kwa kuegemea upande wa kipragmatiki. Leech alilenga kuudara mtazamo wa Grice (1975) kuhusu suala la upole. Kulingana na Leech (1983:132), dhana ya upole ni aina ya tabia ambayo huwawezesha wasemaji na wasikilizaji katika mazungumzo kuhusika katika hali ya mtagusano wa kijamii katika hali ya uiano. Leech anaendelea kufafanua kuwa, jambo muhimu zaidi katika mawasiliano ni kudumisha mazingira mema ambayo yatadumisha mawasiliaano katika muktadha husika.

Leech (1983) anapendekeza kanuni sita za upole ambazo ni: ukarimu, huruma, kujitweza, kumsifu msikilizaji, makubaliano na mkakati. Kwa msingi wa kaida hizi, Leech anapendekeza hali tofauti tofauti ambazo huhitaji aina tofauti za upole. Anaueleza upole kama tabia inayowaruhusu wazungumzaji kuwa katika mtagusano wa kijamii katika mazingira ya utulivu.

Hata kama kanuni hizi za upole kulingana na Leech (1983) zinasaidia katika mawasiliano, zinamlemea msemaji kwani ana jukumu la kuhakikisha kuwa ujumbe umewasilishwa bila kumuuudhi au kumkasirisha msikilizaji. Kwa maoni yetu msikilizaji pia anafaa kuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa mawasiliano yameendelezwa vizuri. Hali ya kujitweza au kumsifu msikilizaji inaweza kumfanya msemaji kunyenyekea zaidi kwa msikilizaji.

Kaida hizi zote huendeleza wazo kuwa upole hasi ni muhimu kuliko upole chanya. Hii ni kwa sababu upole chanya hutumika pale ambapo msikilizaji na msemaji wanajuana kiasi lakini msemaji huzungumza kwa makini ili asiudhuru au asiuaibishe uso wa mzungumzaji. Kwa mfano;

16. Msemaji: Ningependa kula machungwa lakini sina pesa.
    Msikilizaji: Utakula ngapi?

Katika mazungumzo haya msemaji ameomba kununuliwa chungwa kwa unyenyekevu ili asiudhuru uso chanya wa msikilizaji.

Upole hasi hudhihirika wakati msemaji hujihisi kuwa anamsumbua msikilizaji. Msemaji huanza kwa kumtahadharisha kwanza kuwa angetaka kuzungumza naye. Msikilizaji hujaribu kuokoa uso hasi wa msikilizaji kwa kutoingilia uhuru wake. Kwa mfano;

17 Msemaji: Samahani unaweza kunionyesha njia
ya kwenda kwa mweshimiwa
.Msikilizaji: Ndio, una…

Katika mazungumzo haya msemaji alianza mazungumzo yake kwa kuomba msamaha kwanza ndiposa akaendelea kuuliza swali lake kwa msikilizaji.

Kulingana na Leech, kaida zote hazina umuhimu sawa katika mazungumzo. Kaida ya mkakati huathiri tunalosema kwa nguvu zaidi kuliko kaida ya ukarimu. Kaida ya kumsifu msikilizaji ni muhimu kuliko ile ya kujitweza. Kwa hivyo, kuna uwezekano wa kuzingatia kaida zaidi ya moja kwa wakati mmoja katika mazungumzo.

### 2.2.1 Kaida ya Ukarimu

Kaida ya ukarimu inadai kuwa msemaji apunguze uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga manufaa kwake binafsi na azidishe uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga gharama kwake.

18. Msemaji: Ningependa kesho nije kukusaidia kuvuna mahindi.
Msikilizaji: Njoo saa moja asubuhi.

Katika muktadha wa mazungumzo haya, msemaji amelenga gharama kwake kwa kuwa amesema kuwa atamsaidia msikilizaji kuvuna mahindi. Huenda msikilizaji asimlipe au amlipe kwa sababu atakuwa amemsaidia kufanya kazi hiyo.

### 2.2.2 Kaida ya Kumwonea Huruma Msikilizaji

Kaida hii hueleza kuwa msemaji apunguze kutokuwa na huruma kati yake na msikilizaji na azidishe huruma kwa msikilizaji. Kauli katika kaida hii ni aina ya vitendo usemi kama vile kupongeza, kutoa rambirambi na kuhimiza. Kwa mfano;

19. Msemaji: Nasikitika sana kwa kifo cha mwanao.
Msikilizaji: Asante, nishapoa.

Katika mazungumzo haya msemaji anamwonea huruma msikilizaji kwa sababu ya kupoteza mwanawe ndiposa anatoa rambirambi zake kwake. Hata hivyo msemaji anaweza zidisha huruma kwa msikilizaji kwa kumpongeza hata kama hakustahili kupongezwa. Kwa mfano; wakati mtoto anarejea nyumbani na amekuwa nambari ya mwisho shuleni mzazi wake kwa kuwa atataka kumwonea huruma atampongeza kwa kusema,

20. Mama: Hongera sana mwanangu kwa matokeo mema
    Mtoto: Asante sana mama.

Katika mazungumzo haya mama anampongeza mwanawe kwa matokeo bora hata kama alikuwa nambari ya mwisho. Mama amezingatia upole kwa sababu alitaka kuhifadhi uso hasi wa mwanawe kwa kutomwaibisha.

### 2.2.3 Kaida ya Kujitweza

Kaida ya kujitweza hudai kuwa msemaji anafaa kupunguza kauli za kujisifu na azidishe kauli za kujitweza. Katika kaida hii msemaji hafai kusema lolote la kujisifu bali anafaa kumsifu msikilizaji ili apate msaada anaouhitaji. Kwa mfano,

21. Msemaji: Napenda namna unavyopika chapati, si kesho uje unipikie?
    Msikilizaji: Nije saa ngapi?

Mazungumzo haya yanadhihirisha kuwa msikilizaji ni bora kuliko msemaji katika mapishi. Msemaji amejidunisha au amejitweza ndiposa anataka apikiwe na msikilizaji. Katika mazungumzo yao haionekani kuwa msemaji hajui kupika bali huenda ikawa anataka kupikiwa na msikilizaji kwa sababu amechoka au atakuwa na shughuli zingine za dharura.

### 2.2.4 Kaida ya Kumsifu Msikilizaji

Kaida hii hudai kwamba msemaji apunguze uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga kutomsifu msikilizaji na azidishe uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga kumsifu.

Ikiwa kwa sababu moja au nyingine mzunguzaji hawezi kumsifu msikilizaji basi anafaa kutafuta njia nyingine ambazo hazitakuwa na athari chanya. Msemaji anaweza kutumia tasfida ili kuwasilisha ujumbe bila kumkasirisha msikilizaji. Kwa mfano;

22. Msemaji: Funga mlango Moi apite.
    Msikilizaji: (*Anacheka*)…

Iwapo msikilizaji alikuwa amewacha au kusahau kufunga zipu na msemaji anataka kumwarifu afunge zipu bila kuathiri uso wake chanya, atamwambia hivyo kwa kutumia maneno ya tasfida ambayo yatapunguza ukali wa kumwambia moja kwa moja afunge zipu. Kwa kufanya hivyo atakuwa amezingatia upole kwa kuwa atakuwa amehifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kutomwaibisha msikilizaji.

**2.2.5 Kaida ya Makubaliano**

Kaida hii hudai kuwa msemaji anafaa kujiepusha na uwasilishaji wa kauli ambazo huonyesha kutokubaliana. Anafaa kuzidisha uwasilishaji wa kauli ambazo zinaonyesha makubaliano. Kaida hii ni sawa na mkakati chanya wa upole wa Brown na Levinson (1987).

Kaida hizi zinaweza kutumiwa kama mwongozo tu kwa sababu wakati mwingine inakuwa vigumu sana kuepuka kutokubaliana. Kuna sababu nyingi sana ambazo zinaweza kuleta kutokubaliana.

**2.2.6 Kaida ya Mkakati**

Kaida ya mkakati inadai kuwa msemaji apunguze uwasilishaji wa kauli ambazo hulenga kutatiza msikilizaji na kuzidisha uwasilishaji wa kauli ambazo huwa na manufaa kwa msikilizaji. Kaida hii inalingana na mkakati hasi wa upole wa Brown na Levinson wa kupunguza ulazimishaji na mkakati chanya wa upole wa kushughulikia matamanio na mahitaji ya msikilizaji.

Brown na Levinson walidara kanuni ya upole ya Leech na kudai kwamba ilikuwa na mikakati mingi sana. Walisema kuwa kanuni yake haikuwa na ufafanuzi wa kutosha wa kaida ya kiasi, je ni kiasi kipi? Pia hakueleza kama kaida hizi ni bia au zinatumika katika tamaduni mahsusi pekee. Hata kama hakusema kwa maoni yetu kaida hizi huzingatiwa sana katika mawasiliano ya kawaida katika jamii. Si rahisi watu kuwasiliana katika muktadha ambao unaleta ugomvi, na iwapo mawasiliano yao yataleta ugomvi basi watakuwa wamevunja kaida hizi. Ugomvi katika mawasiliano hutokea tu pale ambapo watu wanateta kwa sababu ya jambo fulani kwa kuwa hawajaelewana. Kwa mfano, wakati watu wanataka kumteua kiongozi atakayewawakilisha kila mmoja wao atakuwa na uhuru wa kuchagua yule anayemtaka basi watu wataanza ugomvi kwani kila mtu atapendelea kiongozi wake. Kila mmoja atakuwa na sifa ambazo angependa kiongozi

wake adhihirishe hivyo basi kuzua ugomvi. Kaida za upole huwa zimekiukwa wakati ugomvi huzuka katika mawasiliano.

### 2.3 Nadharia ya Upole ya Brown na Levinson (1987) na Namna Imetumika Kukiuka au Kudhihirisha Upole

Brown na Levinson (1987) walitumia kanuni za Leech (1983) hasa kanuni ya mkakati kuibuka na mikakati minne ya upole ambayo huzingatiwa na msemaji na msikilizaji wakati wa mazungumzo. Mtazamo wa kuhifadhi uso ndio ambao tutatumia sana katika uchanganuzi huu ili kuchunguza mikakati ya upole katika tamthilia ya *Mstahiki Mey*a na kuchunguza namna mikakati hii imetumiwa kuendeleza maudhui na kukuza wahusika. Waasisi wa Nadharia ya Upole ni Brown na Levinson (1987). Ili kubuni nadharia ya upole, walitumia dhana ya uso ya Ervin Goffman (1967).

Kulingana na Goffman, uso ni thamani chanya ya kijamii ambayo mtu hujipa kulingana na mitazamo ambayo wengine huchukulia kuwa imeegemea katika mtagusano wa kijamii. Ndiposa anasema kuwa binadamu ana uso wa hadhira na uso usiokuwa wa hadhira. Hivi ni kusema kwamba binadamu yeyote yule huwa na aina mbili za uso ambazo sharti zithaminiwe na zihifadhiwa katika mazungumzo. Hivi kwamba katika mazungumzo msemaji na msikilizaji saharti wawasiliane bila kudhuruana. Nammna mazungumzo yao yataendelezwa ni sharti yazingatiwe ndiposa nyuso zao zote ziweze kuhifadhiwa. Watafanya hivyo kwa kupongezana na kuhimizana.

Katika kuendeleza dhana ya uso, Brown na Levinson wanasema kuwa kuna uso chanya na uso hasi. Uso chanya ni tamanio la kutaka kukubalika na kuheshimiwa na wanajamii wengine na uso hasi ni tamanio la kutaka kujiwekea mipaka ya uhuru wa kutoingiliwa na kutobaguliwa.

Uso chanya hutaka kutambuliwa na kuheshimiwa. Brown na Levinson wanasema kuwa katika mawasiliano msemaji lazima atumie maneno ambayo hayamuudhi au kumuaibisha msikilizaji. Wanapendekeza kuwa ili kuweza kuhifadhi uso wa msikilizaji au msemaji, ni lazima mikakati ya upole itumiwe. Kwa mfano mkakati wa kuwa nje ya rekodi na mkakati wa kuwa ndani ya rekodi. Wanaeleza kuwa mikakati inayotumiwa inatofautiana kutegemea ni nyuso gani zinazohusika; uso chanya au uso hasi.

### 2.3.1 Vitendo Vinavyotishia Uso

Brown na Levinson (1987:65) wanafafanua kuwa, kuna matendo yanayoweza kutishia nyuso za wasemaji na wasikilizaji katika mawasiliano. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987), kuna aina nne za vitendo vinavyotishia nyuso za wahusika katika mazungumzo. Vitendo hivi huweza kutishia uso wa msemaji au msikilizaji.

Aina ya kwanza ni vitendo ambavyo hutishia uso chanya wa msikilizaji. Vitendo hivi vinaweza kumwaibisha msikilizaji na hivyo kuathiri uso chanya wake. Vitendo hivi ni kama vile; kumtusi, kumdunisha, kumtisha au hata kuzungumzia mada ambazo ni mwiko katika jamii husika. Kwaa mfano msemaji anaweza kuutisha uso chanya wa msikilizaji kwa kumtusi, kwa mfano

23. ‘Urembo wako ni bure ikiwa wewe ni malaya’

Katika mazungumzo haya uso chanya wa msikilizaji umedhuriwa kwa kuitwa ‘malaya’ na msemaji na katika jamii nyingi neon hilo ni mwiko kutaja kutokana na matendo yanayohusika na umalaya. Aidha msemaji anapomtisha msikilizaji huwa pia anadhuru uso chanya wake. Kwa mfano anapomwambia,

24. ‘Unipe pesa zako zote au nikuue’

Kutokana na tishio la kuuawa msikilizaji itabidi ampe msemaji pesa hizo ndiposa asiuawe. Tishio kwa msikilizaji huathiri uso chanya wake.

Vile vile kuna vitendo ambavyo vinatishia uso hasi wa msikilizaji. Vitendo hivi hutokea wakati ambapo msemaji anaingilia uso hasi wa msikilizaji kwa kuamrisha, kutoa onyo, kushauri au hata kutoa maagizo. Kwa mfano, msemaji atatoa agizo kwa msikilizaji kuwa ndiposa msikilizaji amwoe mtoto wa msemaji itabiddi alipe mahari kwanza.

25. ‘Utamwoa mwanangu iwapo utalipa mahari yote’

Vitendo ambavyo hutishia uso chanya wa msemaji ni pamoja na kumwomba msikilizaji msamaha, kukubali pongezi kutoka kwa msikilizaji, kukubali makosa na kujidunisha mbele ya msikilizaji. Kwa mfano,

26 Msemaji: Niwie radhi nimemwaga maji yako.
Msikilizaji: Nimekusamehe.

Katika mazungumzo haya ameanza mazungumzo yake kwa kumwomba msikilizaji msamaha kwa kosa alilolitenda.

Aidha vitendo ambavyo vinatishia uso hasi wa msemaji ni kama vile; kukubali pendekezo kutoka kwa msikilizaji, kukubali kusamehe na kuahidi kitu fulani kwa msikilizaji bila kupenda.

### 2.3.2 Namna ya Kukabiliana na Vitendo Vinavyotishia Uso

Brown na Levinson katika Nadharia yao ya Upole (1987) walipendekeza mikakati mitano ya kukabiliana na vitisho kwa uso wakati wa mazungumzo. Mikakati hii ni; mkakati chanya wa upole, mkakati hasi wa upole, mkakati wa kuwa kwenye rekodi, mkakati wa nje ya rekodi na mkakati wa kukabiliana na vitisho kwa uso kwa kutowasilisha taarifa kabisa.

Unapotumia mkakati chanya wa upole unaonyesha heshima kwa msikilizaji na kuashiria uhusiano baina ya msemaji na msikilizaji. Mkakati hasi wa upole unapunguza ulazimishaji wa taarifa kwa msikilizaji. Mkakati wa kuwa kwenye rekodi hautilii maanani mahitaji yoyote ya uso. Pia huitwa mkakati wa kuwa ndani ya rekodi. Mkakati wa kuwa nje ya rekodi unahusu kuwasilisha taarifa kwa njia isiyo ya moja kwa moja ambapo ni vigumu kuhusisha usemi husika moja kwa moja kwa hivyo kumwacha msikilizaji kufasiri usemi husika jinsi atakavyo. Msemaji anapowasilisha ujumbe wake katika mkakati huu hutumia methali.

Mkakati wa mwisho ni kukabiliana na vitisho kwa uso kwa kutowasilisha ujumbe kabisa. Mkakati huu ndio salama kwa vile una kiwango kikubwa cha upole. Kwa upande mwingine msemaji huwa hatimizi lengo lake la mawasiliano kwa vile ndiposa mawasiliano yakamilike ni sharti msikilizaji atoe wazo lake kwa msemaji. Kwa mfano,

27 Msemaji: Nakuomba uje leo unitembelee nyumbani
Msikilizaji: (*kimya*)

Katika mazungumzo haya, mawasiliano hayajakamilika kwa kuwa msikilizaji ameamua kunyamaza kimya. Ndiposa mawasiliano yakamilike, msikilizaji alifaa kujibu iwapo atafika au la. Kwa mfano,

28 Msemaji: Nakuomba uje leo unitembelee nyumbani.
Msikilizaji: Ndio, nitaja saa nane.

Msikilizaji akijibu hivo, mawasiliano yatakuwa yamekamilika kwa vile msikilizaji atakuwa ametoa maelezo yake.

Mikakati yote mitano hutumika katika mawasiliano lakini mkakati unaotumiwa hutegemea jambo linalozungumziwa, mahali pa mazungumzo, wahusika na muktadha wa mawasiliano. Mikakati hii tumeiangalia kwa undani na tumeeleza jinsi ya kuitekeleza ili kuhifadhi nyuso za wahusika katika mazungumzo.

### 2.3.2.1 Mkakati Chanya wa Upole

Brown na Levinson (1987:101) wanafafanua kuwa, mkakati chanya wa upole huelekezwa kwa uso chanya wa msikilizaji na tamanio lake ni kuwa mahitaji yake yafikiriwe kama ambayo yanatamanika. Kwa kutumia mkakati chanya wa upole, msemaji huashiria kuwa yeye na msikilizaji ni washiriki katika jambo fulani na wote wana msimamo sawa. Hivyo basi mkakati huu hujaribu kupunguza vitisho kwa uso chanya wa msikilizaji kwa kumfanya ahisi vizuri kujihusu na kuhusu matamanio yake.

Msemaji anapotumia mkakati chanya wa upole hujaribu kuwa karibu na msikilizaji kwa kuanzisha urafiki na kumheshimu kwa kumzungumzia mambo ambayo msikilizaji anapendelea. Msikilizaji na mzungumzaji hujaribu kubuni mazingira ambayo yatawatosheleza wote wawili. Mkakati huu hutumiwa katika miungano ya makundi katika jamii. Kwa hivyo, wanajamii huhifadhi na kuendeleza uso chanya zao. Njia zifuatazo hutumika kutekeleza mkakati chanya wa upole;

#### 2.3.2.1.1 Kutumia Ucheshi

Ucheshi hutekelezwa kwa kuzungumzia mambo ya kawaida au yanayojulikana na wazungumzaji. Ucheshi humfanya msikilizaji kuchukulia jambo linalozungumziwa kwa wepesi. Msemaji anapotumia ucheshi katika mazungumzo husaidia kuhifadhi uso chanya wa msikililizaji. Kwa mfano,

29 Msemaji: Nitakununulia gari ukifaulu mtihani.
Msikilizaji: (*Akicheka*) Nitafuahia sana.

Katika muktadha wa mazungumzo haya, msemaji ametumia ucheshi ili kumhimiza msikilizaji kutia bidii katika masomo ili afaulu mtihani wake.

#### 2.3.2.1.2 Kutafuta Makubaliano

Brown na Levinson walieleza kuwa msemaji anaweza kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji kwa kutafuta makubaliano naye. Msemaji ni sharti aibue mada ambazo msikilizaji atakubaliana nazo. Kwa mfano, msemaji anapozungumza na msikilizaji wakubaliane kuhusu mada watakazozungumzia na hii itasaidia kuhifadhi uso chanya wao ambao hautaki kudhuriwa. Msemaji hutumia njia ya kutafuta makubaliano wakati anaelewana na msikilizaji vizuri. Msemaji sharti ajue mambo ambayo msikilizaji anakubaliana nayo na yale ambayo hakubaliani nayo. Kwa maoni yangu njia hii ni mwafaka kwa sababu husaidia kuhifadhi uso chanya wa msemaji na msikilizaji kwa vile mazungumzo yao yatakua juu ya mada ambayo wote wamekubaliana nayo.

#### 2.3.2.1.3 Kuepuka Kutokubaliana

Njia nyingine na kuokoa uso chanya wa msikilizaji ni kuepuka kutokubaliana au kutopingana kwa vyovyote vile na msikilizaji. Msemaji atafanya hivyo kwa kutoa kauli za jumla ndiposa msikilizaji asiweze kuona kuwa msemaji anaegemea upande mmoja. Kwa mfano, msemaji akijua fika kuwa msikilizaji hapendi aina fulani ya tunda atatoa kauli ya jumla na kusema kuwa

30. “Matunda ni nzuri kwa afya ya mwanadamu”

Msemaji amezuia kutopingana na na msikilizaji kuhusu aina ya tunda analopenda au kuchukia kwa kutaja matunda yote kwa jumla.

#### 2.3.2.1.4 Kumtambua na Kumshughulikia Msikilizaji

Katika mawasiliano ni sharti msemaji amtambue msikilizaji na amfanye ahisi vyema. Njia hii ni sawa katika kumpongeza mtu kwa mazuri aliyotenda hata kama ni chakula kizuri alichopika. Kauli za kumsifu msikilizaji huhifadhi uso chanya wake na kumfanya awe na furaha kuwa ametambulika na kukubalika na msemaji. Kwa mfano msemaji anaweza kumtambua msikilizaji kwa kumwambia kuwa,

31. “Umepika chakula kitamu”

Maneno haya yatamfanya msikilizaji kuhisi vyema kwani umemtambua kutokana na jambo jema alilolitenda la kupika chakula kitamu.

#### 2.3.2.1.5 Kuuliza au Kutoa Sababu za Kitendo Fulani

Unapotumia mkakati huu unaepuka kumwamrisha msikilizaji na hivyo kuhifadhi uso wake. Kwa mfano unapomwambia msikilizaji kuwa

32. "Uvutaji wa sigara hudhuru afya ya mwanadamu"

Msemaji katika mazungumza haya ameepuka kumwamrisha msikilizaji kuacha kuvuta sigara badala yake ametoa maelezo kuhusu madhara yanayosababishwa na uvutaji wa sigara ndiposa kupitia kwa sababu za athari za uvutaji sigara msemaji amemtahadharisha msikilizaji na pia amehifadhi uso chanya wake ambao hautaki kuabishwa hadharani.

#### 2.3.2.1.6 Kutumia Vitambulisho vya Makundi

Msemaji pia anaweza kutumia vitambulisho vya makundi kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji. Msikilizaji huhisi vizuri anapotambuliwa kama wanakikundi. Mkakati huu huwa bora wakati msemaji anasifu kikundi fulani ambacho kimetenda mema. Kwa mfano kama msikilizaji ni mmoja kati ya wanasoka fulani ambao wafuzu kutokana na uchezaji wao mwemwa, msemaji atamwambia 'hongera kwa kuwa wachezaji bora' hata kama msikilizaji hakuwa yeye aliye funga bao hilo.

#### 2.3.2.1.7 Kuwa Mrijua

Mkakati huu hutumika wakati wahusika wana uhusiano wa kimamlaka. Msemaji huwa na mamlaka juu ya msikilizaji. Kwa mfano; mzazi na mtoto, mwalimu na mwanafunzi au hata mwajiri na mwajiriwa.

### 2.3.2.2 Mkakati Hasi wa Upole

Brown na Levinson (1987:129), wanaeleza kuwa mkakati hasi wa upole hutumiwa kupunguza ulazimishaji wa kauli fulani katika mazungumzo. Mkakati huu hutumika wakati msemaji anataka kitu fulani kutoka kwa msikilizaji lakini anataka kuhifadhi haki ya msikilizaji ya kukataa. Mkakati huu huendelea kusisitiza tofauti zilizopo baina ya msikilizaji na msemaji. Kwa kuwa msemaji atakuwa akilazimisha matamanio yake kwa msikilizaji basi kuna uwezekano mkubwa wa kumwaibisha. Msemaji atatumia mkakati hasi wa upole kwa njia zifuatazo ili kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji:

#### 2.3.2.2.1 Kutumia Maswali na Vidokezo

Msemaji hutumia mkakati huu ambao ni mkakati hasi wa upole kupunguza ulazimishaji wa kauli fulani katika mazungumzo. Kwa kufanya hivyo, msemaji atamwuliza msikilizaji maswali na kwa kufanya hivyo atakuwa anahifadhi haki yake ya kukataa. Kwa mfano,

33 Msemaji: Je, uliuiba mswada wangu
Msikilizaji: La, hasha.

Katika muktadha wa mazungumzo haya msemaji amehifadhi uso hasi wa msikilizaji kwa kumuuliza swali ndiposa awe na uhuru wa kusema ndio au la.

#### 2.3.2.2.2 Kutumia Vitangulizi

Kitangulizi hutumiwa kwa njia ya kumtayarisha msikilizaji kwa yale anayotaka kusema. Kwa mfano; msemaji akitaka kuwasilisha mambo ambayo anaona kuwa yatamkasirisha msikilizaji ataanza kwa kuomba msamaha,

34. Msemaji: Nasikitika kusema haya, wewe ni mvutaji sigara?
Msikilizaji: (*Anawaza*)

Katika mazungumzo haya msemaji alijua swali atakalouliza msikilizaji ni la kuudhi ndiposa anaanz kwa kuomba msamaha.

#### 2.3.2.2.3 Kuomba Msamaha

Msemaji anaweza kuhifadhi uso hasi wa msikilizaaji kwa kuomba msamaha kabla ya kutoa kauli yake ambayo anafikiria kuwa itamfanya msikilizaji kuaibika au kuhisi vibaya.

#### 2.3.2.2.4 Kutaja Kanuni ya Jumla

Kulingana na Brown na Levinson kutaja kanuni ya jumla humfanya msemaji kutoa kauli inayolenga watu zaidi ya mmoja. Ujumbe hufika bila kuaibisha mtu yeyote iwapo kauli ya jumla itatumiwa. Hii ni kwa sababu kauli hiyo itakuwa ikirejelea kila mtu na sio mtu mmoja mahsusi. Kwa mfano mwalimu akiingia darasani na apate wanafunzi wanapiga kelele atawatahadharisha wote kwa kusema kuwa

35. ‘mkiendelea kupiga kelele nitawachapa’

Hata kama sio wanafunzi wote walikuwa wanapiga kelele awewajumlisa wote ndiposa asidhuru nyuso za wale waliokuwa wakipiga kelele.

#### 2.3.2.2.5 Kuonyesha Heshima Baina ya Msemaji na Msikilizaji

Mkakati huu hulingana na kaida ya Leech ya kujitweza ambayo inasema kuwa msemaji lazima apunguze kauli za kujisifu na azidishe kauli za kujitweza kwa mfano,

36. “Napenda namna unavyopika chapati, si leo uje unipikie?”

Hapa msemaji ametumia kauli ya kumsifu msikilizaji ili afanyiwe anachotaka.

#### 2.3.2.2.6 Kuwa Bila Rajua

Katika mkakati huu msemaji huonyesha kama ambaye hatarajii msaada kutoka kwa msikilizaji japo anauhitaji sana. Mkakati huu hulenga kuhifadhi uso hasi wa msikilizaji.

### 2.3.2.3 Mkakati wa Kuwa Ndani ya Rekodi

Mkakati huu hutumiwa wakati ambapo msemaji na msikilizaji wanafahamiana vyema. Katika mkakati huu msemaji hana jukumu la kuhifadhi uso wa msikilizaji. Kinachotiliwa mkazo ni ujumbe unaopaswa kuwasilishwa wala sio mahitaji ya kuhifadhi uso. Mkakati huu hutumiwa katika mazingira yafuatayo;

#### 2.3.2.3.1 Katika Hali ya Dharura au Kutamauka

Mkakati huu wa kuwa kwenye rekodi hutumiwa wakati ambapo kuna hali ya dharura au ya kutamauka. Msemaji hushughulika na manufaa kwa msikilizaji wala sio kuhifadhi uso. Mfano wa hali hii ni wakati ambapo Daktari Siki anamweleza Waridi kuwa wagonjwa wakiendelea kungoja dawa, ugonjwa nao utasubiri. Kile Siki anarejelea ni kwamba hakuna dawa hospitalini na watu wataendelea kufa kwa sababu ya ukosefu wa dawa. Mkakati wa kuwa kwenye rekodi umezingatiwa.

#### 2.3.2.3.2 Kutoa Ahadi kwa Msikilizaji

Mkakati wa kuwa kwenye rekodi pia unaweza kutumiwa wakai ambapo msikilizaji anaahidiwa kita fulani. Katika hali hii msemaji hana haja ya kuhifadhi uso wa msikilizaji kwa kuwa ahadi hizo zitakuwa na manufaa kwa msikilizaji. Kwa mfano, Meya Sosi anapoahidi kwamba

37. ‘dawa zipo bandarini zitawasili’

wanacheneo wanasubiri kwa hamu kwa vile wanajua kwamba dawa hizo zitakuwa za manufaa kwao. Hapa mwandishi kupitia kwa mhusika Meya ametumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi ili kuhifadhi uso chanya wa msikilizaji. Kwa hivyo mkakati wa kuwa kwenye rekodi umezingatiwa.

**2.3.2.3.3 Tofauti za Kimamlaka Kati ya Msemaji na Msikilizaji**

Mkakati huu wa ndani ya rekodi hutumiwa wakati msemaji na msikilizaji wako katika kiwango tofauti kimamlaka. Brown na Levinson walitambua viwango vya kisosholojia ambavyo watu huteua viwango vya upole na pia kukadiria athari ya vitisho vya nyuso zao. Mzazi anapozungumza na mwanawe hahitaji kuzingatia upole lakini mtoto akizungumzia mzaziwe anastahili kuzingatia upole. Tofauti za kimamlaka zinazingatiwa katika mazungumzo kati ya Meya na Dida. Tofauti hii inadhihirika wakati inaonekana kuwa Dida amemchoma Meya na chai aliyokuwa ameitia chupani kama kawaida. Aidha Siki anapomwuliza mamake Dadavuo Kaole kuhusu umri na chakula alichompa mwanawe, anatumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Mama huyo anaonekana kujibu maswali yake Siki moja kwa moja kwa vile Siki anatumia mkakati wa kuwa kwenye rekodi kutaka kujua chanzo cha ugonjwa huo. Kwa hivyo mkakati wa upole wa kuwa kwenye rekodi umezingatiwa katika mazungumzo kati ya Siki na mamake Dadavuo Kaole.

38. Siki: (*Anaelekea kwa mama. Anamgusa mtoto.*) Ana nini mtoto?
Mama**:** Sijui. Naona anaendesha tu!
Siki: Tangu lini hali hii?
Mama: Jana jioni baada ya chajio.
Siki: Jina?
Mama: Dadavuo Kaole
Siki: Umri?
Mama: Miaka mitatu.
Siki: (*Akimtazama mama*.) Ulimlisha nini?
Mama: Chakula.(UK 4)

Mazungumzo haya kati ya Siki na mamake Kaole yamezingatia mkakati wa kuwa ndani ya rekodi. Siki anamwuliza maswali ya moja kwa moja ndiposa aweze kumsaidia mtoto Kaole.

#### 2.3.2.3.4 Katika Kitendo cha Kumfaidi Msikilizaji

Mkakati huu wa kuwa kwenye rekodi pia hutumiwa wakati tendo linalozungumziwa huwa la kumfaidi msikilizaji.

### 2.3.2.4 Mkakati wa Kuwa Nje ya Rekodi

Katika mkakati huu msemaji halazimishi matamanio yake kwa msikilizaji bali hudokeza tu jambo fulani na kumwacha msikilizaji aufasiri ujumbe husika jinsi apendavyo. Msemaji huwa hatoi ujumbe wake moja kwa moja. Brown na Levinson (1987:211) wanasema kuwa sio rahisi kuhusisha lengo moja wazi katika usemi husika. Utata huu unaafikiwa kwa kuvunja kanuni za Grice za uhusiano na idadi na hivyo kumwacha msikilizaji kufasiri maana ya umaanisho. Uso chanya wa msikilizaji huweza kuhifadhiwa iwapo utapata maana halisi ya ujumbe uliosemwa na msemaji. Katika hali hii msemaji anaweza kukana kusema kauli husika kwa vile msikilizaji alijitafsiria ujumbe huo mwenyewe. Kanuni hii hutumiwa sana na wanasiasa. Kwa kuwa msikilizaji anaweza kutafsiri ujumbe husika visivyo, matumizi ya mkakati huu huwa na changamoto si haba. Msemaji kwa hivyo huwa hajatimiza lengo lake katika mawasiliano yake.

Kulingana na Brown na Levinson, ni salama kutumia mkakati huu katika mawasiliano lakini msikilizaji huchukua muda mrefu kutafsiri ujumbe wa msemaji. Mkakati huu huweza kutumiwa kwa njia zifuatazo;

#### 2.3.2.4.1 Kutumia Kejeli au Kinaya

Kinaya hutumiwa katika mkakati wan je ya rekodi ili kuhifadhi nyuso za wazungumzaji. Njia hii hutumiwa wakati ambapo msemaji hataki kusema jambo moja kwa  moja. Uteuji wa waneno wafaa kuzingatiwa wakati ambapo mtu anatumia mkakati huu wa kuwa nje ya rekodi. Hii ni kwa sababu msikilizaji anweza tafsiri maneno hayo visivyo, kwa hivyo msemaji hataafika lengo lake.

Katika mawasiliano kati ya Meya na Daktari Siki, Meya anasisitiza kuwa lazima aitwe 'Mstahiki Meya' akishikilia kuwa kama kiongozi wa Baraza la Cheneo, hilo ndilo jina ambalo kila mkazi wa eneo hilo alipaswa' kumtambua' kwalo. Anamwambia Siki, "pamoja na salamu zako, ni mpaka unite Sosi? Wewe tu ndiye hujui kuwa mimi ndiye Meya wa Baraza la mji wa Cheneo.

39. Siki: Habari za leo ndugu Sosi?
Meya: (*Anamtazama kwa muda*) Hivi uzionavyo. (*Kimya*)
Pamoja na salamu zako, ni mpaka unite Sosi?

Wewe tu ndiye hujui kuwa mimi ndiye Meya wa Baraza
la mji wa Cheneo? (UK 10)

**2.3.2.4.2 Kutumia Vidokezo**

Mkakati huu hutekelezwa kwa kutumia vidokezo. Msemaji hutoa vidokezo kuhusu jambo ambalo angetaka msikilizaji atekeleze. Msemaji huwa hataki kusema jambo hilo moja kwa moja. Kwa mfano, Siki anapoenda kwa Meya sosi kumweleza namna maisha ya watu waliomchagua yamekuwa ngumu hadi wameshindwa kumudu gharama za matibabu na dawa zenyewe hakuna. Aidha gharama za maisha zinazidi kupanda kila uchao na mahitaji nayo yanazidi kuongezeka ilhali mishahara haipandi. Kutokana na vidokezo hivi Siki alitaka kueleza kuwa ilikuwa ni sharti Meya awalipe wafanyakazi wa Baraza la mji mishahara yao.

40. Siki: …. Sikiliza Sosi. Hizi si habari za kugoma au kutogoma.
La hasha! Ni habari za hali ya maisha ya watu waliokuchagua
wewe kwa kuamini kuwa utaziboresha hali zao.
Watu wanakulilia. Wanataka uwasikilize.
Hali yao ya maisha ni ngumu. Wanashindwa
kumudu gharama za matibabu na dawa zenyewe
hakuna. Gharama za maisha zinazidi kupanda na
mahitaji nayo yanazidi kuongezeka ilhali
mishahara haipandi…(UK 11)

Vidokezo hivi ambavyo Siki anadokeza ni mbinu ya kuwa nje ya rekodi. Siki alidhamiria kumweleza Mstahiki Meya kuwa yafaa awalipe wafanyakazi wa mji wa cheneo mishahara yao.

**2.3.2.4.3 Kutumia Maswali ya Balagha**

Maswali ya balagha ni maswali ambayo msemaji huwa hatarajii majibu kutoka kwa msikilizaji. Maswali haya huwa na majibu ambayo yako wazi. Maswali haya yanapotumiwa huibua hisia fulani. Msemaji huwa na majibu ya maswali haya anapouliza msikilizaji katika mazungumzo. Maswali haya hutumiwa kutilia mkazo jambo linalosemwa na msemaji au jambo linalozungumziwa na msemaji na msikilizaji. Mhubiri anapomwuliza Meya kuwa;

41. Meya: Mara baada ya maombi yako.
Mhubiri: Kweli kilio chetu kiliskika pale pale.
Nani atakuchezea? (UK 43)

Swali hili ambalo mhubiri anauliza Meya limekiuka upole kwa vile linarejelea mambo ambayo ni nje ya rekodi.

**2.3.2.4.4 Kuzua Utata**

Kuzua utata ni kusema jambo kwa njia isiyoeleweka. Katika mkakati huu, msikiliazaji huwa na jukumu la kutafuta fasiri ya jambo linalorejelewa na msemaji.

**2.3.2.4.5 Matumizi ya Sitiari**

Sitiari ni mbinu ya kulinganisha kitu kimoja na kingine kimoja bila kutumia viunganishi au vihusishi fulani. Sitiari inapotumiwa katika mawasiliano, hujenga picha au taswira akilini mwa msemaji na msikilizaji. Kwa mfano, ninaposema kuwa 'babangu ni simba' nina maana kuwa babangu ni mkali sana sio wa kupenda mzaha. Mbinu hii hutumiwa kuonyesha upole kwa sababu ni njia ya kuwa nje ya rekodi. Siki anawalinganisha raia walioudhika na punda aliyeudhika. Punda inarejelea raia amboa wanafanya kazi bila kupokea mishahara yao. Raia hawa pia wanalipwa mishahara duni na mishahara yao kucheleweshwa.

42. Meya: …Naona unajaribu kutia kidole chako katika
mzinga wa nyuki. Ni hatari
Siki: ….Kama huku si kuwatusi wananchi basi
ndio kutembea nyuma ya punda aliyeudhika. (UK 14)

Aidha, Meya moja kwa moja anamwita Diwani wa III sumu. Neno sumu linamrejelea diwani huyu kwa kuwa ndiye wanayeshirikiana na Siki kutetea haki za wanacheneo. Meya wa cheneo katika mazungumzo yake na Diwani wa II wanatumia mkakati wa kuwa nje ya ya rekodi. Kwa mfano,

43. Meya: ….Akilipata hili basi atakuwa amepata
fursa ya kuwachochea watu kufanya
maandamano. Lazima kwanza mnihakikishie
kuwa huyo sumu hapati hata fununu
ya jambo hili. Hii ni bomu inayoweza
kutulipukia usoni. (UK 62-63)

#### 2.3.2.5 Mkakati wa Kukabiliana na Vitishio kwa Uso kwa Kutowasilisha Taarifa Kabisa

Msemaji huamua wakati mwingine kunyamaza kimya kwa kutotoa au kutowasilisha taarifa yoyote. Njia hii ni mwafaka lakini msikilizaji huwa amejiwacha katika hali ya taharuki kwani hajui sababu za kumfanya msemaji kuamua kunyamaza kimya. Msemaji huwa amekabiliana na vitishio vyote vya uso. Mkakati huu ndio ulio na kiwango kikubwa cha upole.

## 2.4 Hitimisho

Katika sura hii tumechanganua namna mikakati ya upole inavyotumiwa kujenga ushirikiano baina ya msemaji na msikilizaji katika mawasiliano. Tumechanganua kanuni za ushirikiano za Grice (1975) ambazo ni kanuni ya ubora, kanuni ya idadi, kanuni ya uhusiano na kanuni ya namna. Tumeona kuwa katika mawasiliano ni vyema kanuni hizi kuzingatiwa ndiposa mawasiliano yaweze kukamilika.

Aidha tumechanganua namna Leech (1983) alivyochanganua kanuni zake za upole. Kulingana na Leech kanuni kama vile za ukarimu, kumwonea huruma msikilizaji, msemaji kujitweza, kumsifu msikilizaji na kukubaliana lazima zizingatiwe katika mazungumzo ndiposa uso hasi wa msemaji na msikilizaji uweze kuhifadhiwa. Tumechanganua namna Brown na Levinson (1987) kupitia kwa Nadharia ya Upole walivyopendekeza kuhusu njia za kukabiliana na vitendo vinavyotishia uso wa msikilizaji na msemaji.

# SURA YA TATU

# NAMNA TAMATHALI ZA USEMI ZINAVYODHIHIRISHA UPOLE KATIKA TAMTHILIA YA MSTAHIKI MEYA

## 3.0 Utangulizi

Katika sura hii tutachanganua namna tamathali mbalimbali za usemi zilivyotumiwa ili kudhihirisha au kukiuka upole katika tamthilia ya *Mstahiki Meya.* Katika uchanganuzi wetu tutaegemea katika semantiki kwa sababu hili ni tawi linalojihusisha na kuchunguza lugha katika kiwango cha maana. Semantiki huchunguza maana ya maneno yanayopatikana katika lugha yoyote ile. Katika sura hii tutachanganua namna mwandishi alikiuka matumizi ya lugha ya kawaida ili kudhihirisha au kukiuka upole. Tamathali za usemi tutakazozingatia ni kama vile; tashhisi, sitiari, majazi na maswali ya balagha.

## 3.1 Majazi

Kulingana na Wamitila (2008) majazi ni mbinu ya kuwasawiri wahusika kando na mbinu ya: maelezo ya mwandishi, maelezo ya wahusika wengine na matumizi ya mazungumzo. Mbinu hii pia hutumika kutaja mahali fulani kulingana na namna au jinsi mahali hapo panavyoonekana na kuhusu tabia au sifa za watu wanaopatikana katika mahali hapo. Kwa upande wa wahusika, mwandishi huwapa majina yanayoambatana na matendo yao, sifa zao na tabia zao. Wasomaji basi huweza kutambua tabia na wasifu wa mhusika kwa urahisi zaidi.

Wasomaji wa kazi ya fasihi hulazimika kuridhika na uamuzi au maamuzi ya mwandishi. Mwandishi ana uhuru wa kuteua majina ya wahusika apendavyo na majina ya mahali katika uandishi wake. Mifano ya majazi katika tamthilia hii ni kama ifuatavyo;

### 3.1.1 Sosi

Sosi ni jina ambalo limetoholewa kutoka neon la kiingeereza ‘sause au source’ na linamaaanisha kula au kubugia vyakula fulani au chanzo cha jambo fulani. Sosi ni meya wa baraza la mji wa Cheneo. Kulingana na tabia zake yeye ni mhusika anayetumia mamlaka yake ‘kula’ mali ya wanacheneo. Jina hili Sosi limetumiwa kijazanda kuashirai kuwa anatumia mali ya baraza visivyo. Sosi anawapeleka wanawe ng’ambo kusomea huko wakitumia pesa ya baraza la mji

badala ya Meya kutumia pesa hizo kuboresha viwango vya elimu ya Cheneo. Aidha, anampeleka mkewe ng'ambo kujifungulia huko badala ya kuweka dawa hospitalini.

44. Siki: Habari za leo ndugu Sosi?
Meya: …Hivi uzionavyo. (*Kimya*) Pamoja na salamu zako, ni mpaka unite Sosi?... (UK10)

Jina hili la majazi Sosi limedhihirisha mkakati wa kuwa nje ya rekodi unaodai kuwa msemaji asiseme maneno moja kwa moja bali atumie mafumbao au njia ya mzunguko kueleza jambo fulani. kwani sisi kama wasomaji ndio tunatambua kuwa Meya alikuwa 'akisosi' mali ya baraza la Cheneo.

Sosi ni jina ambalo laweza kuwa na maana ya kuwa ni chanzo cha jambo fulani. Jina hili limetoholewa kutoka jina la kiingereza 'source.' Sosi ni chanzo cha shida na matatizo yote ambayo wanacheneo wanapitia. Kwa mfano, kutokana na matumizi yake mabaya ya pesa za baraza la mji wa cheneo, wafanyakazi wa mji huo wanagoma kwa sababu ya kucheleweshwa mishahara, kutolipwa mishahara yao na kulipwa mishahara duni. Kwa hivyo jina hili limedhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi kwa vile anayotenda kiongozi huyu ya uhusiano na jina lake.

### 3.1.2 Siki

Jina hili lina maana kuwa ni hali ya kutafuta mwafaka fulani kutokana na jambo fulani linalowakabili watu fulani. Jina hili linatokana na jina la kiingereza 'seek' lenye maana ya tafuta. Siki ni daktari katika hospitali ya chaneo. Siki alikuwa mstari wa mbele kusaidia wafanyakazi wa baraza la mji wa Cheneo kutafuta haki yao. Anamwelezea Meya kuhusu changamoto wanazokumbana nazo lakini Meya ametia dawa kwenye sikio lake. Anajaribu kutafuta suluhu mwafaka kutokana na mgomo wa wafanyakazi wa baraza la Cheneo.

Jina hili limedhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa ndani ya rekodi ambao unadai kuwa msemaji aseme maneno moja kwa moja bila kulenga kuhifadhi uso wa msikilizaji. Ujumbe wa msemaji kwaa msikilizaji uwe ule wa kueleweka haraka kwa vile kazi ya Siki ilikuwa ni kuwasaidia wanacheneo ili waweze kujimudu kimaisha kutokana na gharama za maisha ambazo zinapanda kila uchao.

### 3.1.3 Kheri

Jina Kheri linamaanisha jambo au kitu kuwa 'bora' Kheri ni Diwani III wa baraza la mji wa Cheneo. Diwani huyu aliwatakia mafanikio njema wananchi wa mji wa cheneo ndiposa anajaribu kutetea haki zao. Hana uwezo wa kujikomboa na kukomboa wanacheneo kutoka kwa nyororo ya ufisadi. Sababu kuu ikiwa alikuwa ametengwa na Meya pamoja na madiwani wengine. Ndiposa uamuzi wote katika baraza la mji wa Cheneo unafanywa na Meya, Bili, Diwani I na Diwani II.

45. Siki: Unaweza kufanya jambo.
Diwani III: Lipi la kufanywa?
Siki: Kheri, wewe ni diwani kama huyo Meya Sosi na mnakutana kila leo….

Katika mazungumzo haya Siki anajaribu kumweleza Kheri na kumuhimiza aendelee na harakati zake za kukomboa mji wa Cheneo. Mkakati ambao umetumika katika jina hili ni mkakati wa kuwa ndani ya rekodi kwa vile Siki hakutaka kuokoa uso wa Meya baali alitaka kutetea haki za wanacheneo. kwa vile jina hili linatoa sifa halisi za mhusika huyu pamoja na tabia zake kwa jumla.

Kuna majina mengine ya kimajazi ambayo yamejitokeza katika tamthilia hii ya *Mstahiki Meya* kwa jumla. Bwana usalama alipewa jina hilo kwa vile alishughulikia maswala yote ya usalama katika mji wa cheneo. Bwana uchumi na kazi alishughulikia maswala yote ya kiuchumi na biashara katika mji huo. Vile vile hoteli ya 'kajifahari' ni jina la kimajazi ambalo lina maana ya kujistarehesha. Mhubiri kwa upande mwingine alipewa jina hilo kwa kuwa kazi yake ilikuwa ni kueneza injili. Kwa jumla majazi ni mbinu ambayo inadhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa ndani ya rekodi hivyo basi kudhihirisha matumizi ya kanuni za ushirikiano za Grice (1975) ambazo ni; kanuni ya uhusiano, kanuni ya idadi, kanuni ya ukweli na kanuni ya namna. Majina yote ya wahusika na mahali yanadhihirisha uhusiano uliopo baina ya jina lenyewe na matendo ya wahusika hao. Majina haya yana ukweli fulani ambao unaweza dhibitishwa. Kwa mfano ukweli kuwa Bwana Kheri ni kiongozi wa uhusiano mwema unaweza dhibitishwa kupitia kwa namna anashirikiana na wanacheneo na namna anajaribu kutetea haki za wanacheneo.

### 3.1.4 Cheneo

Neno cheneo linatokana na neno –enea ambalo lina maana ya kuenea kwa jambo au kitu fulani. Mji wa Cheneo ulikuwa na matatizo mengi ambayo yalikuwa yameenea kote. Aidha kulikuwa na harufu mbaya ambayo ilikuwa imeenea kote. Harufu hii ilitokana na taka ambazo zilikuwa zimetapakaa kote kwa sababu ya mgomo wa wafanyakazi wa baraza la mji. Jina hili la kimajazi limetumia mkakati wa ndani ya rekodi kwa vile tunapata kuona sehemu ambayo imeenea kwa kila aina ya uovu.

Kwa jumla, kupitia mbinu hii ya majazi mwandishi wa tamthili hii ameweza kudhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa ndani ya rekodi kama ilivyopendekezwa na Brown na Levinson (1987). Utafiti huu umedhihirisha matumizi ya majina ya wahusika kwa njia ya moja kwa moja kutokana na sifa zao. Kupitia utafiti huu mtafiti anafahamu kile Meya alikuwa 'akisosi' na kile Siki alikuwa akitafuta, yaani Meya alikuwa anatumia pesa za baraza visivyo na Siki alikuwa akijaribu kutafutia wanacheneo hasa wafanyakazi wa baraza la mji wa Cheneo haki zao.

Aidha utafiti umedhihirisha kile ambacho kilikuwa kimeenea katika mji wa Cheneo. Kulikuwa na ufisadi uliokuwa umeenea kote na uliendelezwa na vingozi kama vile madiwani na Meya wa baraza. Vile vile kulikuwa na umaskini ambao pia ulikuwa umeenea sababu kuu ikiwa hali ya maisha katika mji huo ilikuwa imepanda na wafanyakazi walikuwa wanalipwa mishahara duni kando na kucheleweshwa mishahara yao.

Pia kanuni ya ukweli, ubora, uhusiano na namna kulingana na Grice (1975) zimedhihirika kupitia matumizi ya majazi. Kwanza kabisa ni ukweli kuwa Meya aliitwa 'sosi' kwa kuwa alikuwa 'akisosi' pesa za baraza la mji. Katika utafiti wetu tuliweza kudhibitisha kuwa alitumia mali ya baraza visivyo. Jina hili ni bora kabisa kwake kwa vile linadhihirisha kile alichokuwa akifanya kama kiongozi wa wanacheneo. Jina hili pia limetumiwa kwa namna iliyo sawa kwa vile limetumiwa kwa namna iliyo wazi na lina uhusiano na kile alichokuwa akitenda Meya.

## 3.2 Sitiari

Kulingana na Wamitila (2008), sitiari ni tamathali ya usemi ya ulinganishi usiotumia vilinganishi 'kama', 'mithili', 'ja', 'mfano wa' n.k. Anaendelea kusema kuwa dhana ya sitiari inatawala situ mazungumzo bali maandishi kwa kiasi kwamba inafaa ichunguzwe pekee badala yakujumlishwa na taamathali nyinginezo. Kwamba kulingana naye msingi wa sitiari ni uhamishi wa maana.

Kwa mfano tunaposema kuwa, 'baba ni mlingoti' pana uhamisho wa maana (baba kupewa sifa ya mlingoti). Sitiari ni mbinu ya kulinganisha kitu kimoja na kingine kwa njia ya moja kwa moja. Matumizi ya sitiari huhitaji msomaji kuchambua maana ya ndani iliyokusudiwa na mwandishi fulani wa kazi ya fasihi. Kwa mfano mtu anaposema kuwa

46. 'baba yangu ni simba,'

haimaanishi kuwa baba yake amegeuka na kuwa simba bali anamaanisha kuwa babake amekuwa na tabia kama za simba kama vile kuwa mkali sana.

Sitiari inapotumika hujenga picha au taswira fulani katika akili ya wasomaji, wakataka kujua mwandishi alikusudia kusema nini anapotumia maneno fulani. Sitiari huwa na maana nyingine ambayo hutakiwa kufasiriwa kando na ile maana ya kijuujuu. Mwandishi ametumia mbinu hii kudhihirisha au na kukiuka upole.

Meya anamwambia Siki kuwa anajaribu kutia kidole kwenye mzinga wa nyuki. Meya anajilinganisha na nyuki ambao ni wadudu hatari sana hasa kwa maisha ya binadamu. Katika usemi huu, mzinga wa nyuki imetumika kijazanda. Binadamu yeyot ule anapojaribu kuweka vidole katika mzinga wa nyuki, wataumwa na nyuki wale na wamuangamize kabisa.

47. Siki: Ni kweli kuna utulivu lakini utulivu
wenyewe unatokana na watu wenyewe
kutopenda matata.
Meya: (*Ameudhika.*) Siki, naona bado ule utundu
wa utotoni haukukutoka. Naona
Unajaribu kutia kidole chako katika mzinga
wa nyuki. Ni hatari. (UK14)

Meya anamtahaadharisha Siki kuwa yeye ni nyuki na atamwangamiza namna nyuki wanavyoangamiza wanadamu. Mkakati wa kuwa nje ya rekodi umetumika hivi kwamba neno 'nyuki' limetumiwa kurejelea ubaya au uovu alionao Meya na sasa anaweza tumia mamlaka yake kumwangamiza Siki.

Siki anatahadharishwa kuwa, akijaribu kupinga hatua anazopiga Meya atakuwa kwenye hatari. Maneno 'simba mwenye watoto,' yametumiwa kurejelea hatari. Simba mwenye watoto hawezi kukamuliwa maziwa kwa vile ni mkali sana.

48 Siki: …Mnajifikiria tu. (*Kimya*.) Kama huku si
kuwatusi wananchi basi ndio
kutembea nyuma ya punda aliyeudhika.
Meya: (*Kwa ukali*.) Hapa ni kwangu Siki.
Unifuate kwangu unitusi…Sisi tuna
malengo ya millennia…Kupinga
haya ni sawa na kumkama simba mwenye
watoto.(UK 14)

Mwandishi kupitia kwa mhusika Meya ametumia mkakati wa nje ya rekodi kwa kuwa itamlazimu Siki kufasiri kile Meya alikuwa akirejelea akisema kumkama simba mwenye watoto. Meya kwa upande mwingine alitaka kuhifadhi uso hasi wa Siki ambao hautaki kuingiliwa kwa kuwa tayari amudhika na utendakazi wa Meya Sosi.

Bwana Kheri naye anendeleza matumizi ya jazanda anapolinganisha cheneo na mataifa mengine yanayoendelea kuwa ‘kaka zetu.’

49 Meya: Bwana Uchumi na Kazi unakusudia nini?
(*Anamtazama kwa ukali*.) Wewe
kwanza una mipango gani katika kitengo chako?
Diwani III: Siuoni mpango wa kuwanufaisha watu wetu.
Watu wengi hawana ajira.
Walio nayo mishahara yao haitoshi wala
hailipwi kwa wakati. Zaidi yaa hilo
tumelazimishwa na kaka zetu kupunguza
idadi ya wafanyakazi. Kaka zetu hao
hawaajatolea hela za mkopo
na hivyo sisi hatuwezzi kuwapa ahadi
ya kuwaongeza watu mishahara….(UK 20)

Neno hili halijatumiwa kurejelea kaka ndugu wa kiume bali ni kaka mataifa ambayo yanaendelea kama vile cheneo. Mwandishi katika muktadha huu ametumia mkakati wa kuwa nje ya rekodi ili kumfanya msomaji wa kazi yake kujifasiria maana ya ndani ya maneno au jazanda hilo.

Bili, ambaye ni rafikiye Meya, anamwambia Meye kuhusu wafanyakazi wa Cheneo ambao wamegoma. Anawapa jina la ‘debe tupu’ ambalo kwa kawaida hupiga kelele sana. Huu ni mkakati wa kuwa nje ya rekodi kwa vile anawalinganisha wafanyakazi na debe linalopiga kelele.

Katika kuichanganua mbinu hii ya majazi tuliweza kutambua kuwa mwandishi aliweza kukiuka kanuni za upole kulingana na Grice (1975) ambazo ni; kanuni ya namna, kanuni ya idadi, kanuni ya uhusiano na kanuni ya ukweli au ubora. Mbinu hii ya jazanda imeweza kutumiwa kwa namna

ambayo ni tata mno. Ni sharti msomaji au mtafiti aweze kuisoma kazi hii kwa kina mno ndiposa aweze kugundua kile mwandishi aliweza kudhamiria.

Idadi ya maneno yaliyotumiwa ni chache kulingana na Grice (1975) ambapo anasema kuwa msemaji asememe maneno machache yanayoweza kueleweka kwa urahisi. Ndiposa tuweze kuelewa kile mwandishi alikuwa anamaanisha anapotumia jazanda, tuliweza kuzingatia muktadha wa maneno yaliyosemwa. Kwa mfano, Bwana Kheri anapolinganisha Cheneo na mataifa mengine anatumia neon ‘kaka zetu’. Katika muktadha huu alikuwa anarejelea mataifa kama Cheneo na wala sio kaka ndugu wa kiume.

Matumizi ya jazanda aidha hayana uhusiano wa moja kwa moja na kile kilichokuwa kikirejelewa. Kwa hivyo mbinu hii pia imekiuka kanuni ya uhusiano kulingana na Grice (1975). Kwa mfano hakuna uhusiano uliopo kati ya mwanadamu na debe. Meya anaposema kuwa wafanyakazi wa Cheneo ni ‘debe tupu’ tunapata maana yake kulingana na muktadha wa mawasiliano yao ambapo walikuwa wanarejelea wafanyakazi ambao wamegoma.

Pia mbinu hii kwa kiasi fulani imekiuka kanuni ya ukweli au ubora kwa vile hatuwezi kudhibitisha kile ambacho kilikuwa kinarejelewa na mwandishi kupitia kwa wahusika wake. Ukweli ni kwamba maneno kama vile kusema kuwa ‘kukama simba mwenye watoto’ hatuwezi tukadhibisha ukweli wa maneno haya kwa kuwa hatujui huyu simba mwenye watoto atafanya nini ukimkama.

### 3.3 Maswali ya Balagha

Maswali ya balagha ni mbinu ambayo mwandishi katika kazi yake hutumia maswali ambayo hayahitaji majibu. Maswali haya huwa hayahitaji majibu kwa sababu majibu yake huwa wazi kwa msomaji. Mbinu hii ya kutumia maswali yasiyohitaji majibu ni mwafaka au bora kwa sababu humfanya msomaji kufikiri kuhusu wazo, hali au jambo fulani ambalo tayari lilikuwa limetajwa hapo awali. Maswali yafuatayo tutayachanganua kwa misingi ya mikakati ya upole ili kubaini iwapo mikakati ya upole imekiukwa au na imedhihirishwa na ni kwa sababu gani.

Mey Sosi anamwuliza Siki swali balagha kuwa,

"Huoni kuwa Cheneo ni kisiwa cha kupigia mfano"

50. Siki: …Yapo mabaraza yaliyoendelea na kufikia
upeo wa kuendelea na bado hayakukomea hapo.
Yanahitaji kupiga hatua mpya kila uchao.
Meya: (Anamtazama kwa ukali.) Wewe tu ndiye
huoni tuliyoyafanya na
tunayoendelea kuyafanya. Utatosheka lini wewe?
Huoni kuwa Cheneo ni kisiwa cha kupigia mfano?
UK11

Maswali ya balagha yaliyotumiwa katika mfano huu ni;

51 "Utatosheka lini? na "Huoni kuwa cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano"

Swali hili balagha linadhihirisha matumizi ya mkakati nje ya rekodi unaodai kuwa msemaji awasilishe ujumbe kwa njia ya kimafumbo, yaani njia isiyo wazi. Cheneo sio kisiwa cha kupigiwa mfano kwa kuwa kuna ufisadi mno unaoendelezwa na viongozi.

Tunajua kuwa Cheneo si kisiwa cha kupigiwa mfano kwa sababu hali ya maisha ni ngumu, wanacheneo wameshindwa kumudu gharama za matibabu na dawa hakuna katika hosspitali. Hii ndio sababu kuwa swli hili halihitaji jibu kwa vile kupitia kwa usomaji tunapata kutambua aina ya kisiwa cha cheneo ambacho sio cha kupigiwa mfano. Meya alitaka kuudhuru uso hasi wa Siki ambao tayari ulikuwa umedhurika kutokanaa na matendo ya Meya ya kifisadi.

Kwenye mazungumzo kati ya Meya na Bili, maswali ya balagha yamedhihirika. Muktadha wao wa mazungumzo unadhihirisha sababu tosha na wazi kuwa yeye kama kiongozi hajawajibika ipasavyo. Kwa mfano;

52 Bili: Sikujua. Hata mimi sasa naona nitamtuma
mke wangu huko huko wakati wake
ukitimia. (Kimya.) Wewe bwana siku hizi
lazima una pesa licha ya hali ngumu.
Meya: Nisipokuwa nazo, nani atakuwa nazo?
Mimi nimeuza vipande vyangu vitatu
vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii.(UK 27)

Katika muktadha wa mazungumzo haya, swali balagha linalodhihirisha Upole ni;

53.“Nisipokuwa nazo, nani atakuwa nazo”

Swali hili limedhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi unaodai kuwa msemaji awasilishe ujumbe wake kwa njia ya moja kwa moja na iliyo wazi. Meya anadai kuwa asipokuwa na pesa nani atakuwa nazo. Amesema haya kwa njia iliyo wazi kabisa kwa namna alivyosema na maneno haya ni kweli na yana uhusiano na kile anachotendea wanacheneo. Hivyo basi maneno haya yamedhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi.

Meya anajidai kwa Bili kuwa, yeye hawezi kosa pesa za kumpeleka mkewe kupata matibabu kule ng’ambo. Njia za Meye za kupata pesa si wazi ndiposa mwandishi anatueleza kuwa alikuwa ameuza vipande vitatu vya ardhi na alikuwa amebakiza vitano *incase*.

Tukizingatia kanuni za Grice (1975), maswali ya balagha yamedhihirisha baadhi ya kanuni kama vile kanuni ya idadi, kanuni ya namna, kanuni ya uhusiano na kanuni ya ukweli.. Tuliweza kuona kuwa maswali haya yalikuwa na uhusiano nay ale yaliyokuwa yamesemwa hapo awali. Pia maswali haya yanaweza dhibishwa ukweli wake hata kama yamedhihirisha mkakati wa kuwa ndani ya rekodi. Idadi ya maneno yaliyotumiwa ni sawa na hivyo maswali haya yanaweza eleweka moja kwa moja. Yametumiwa kwa namna iliyo wazi kiasi kuwa tumechanganua maana yake.

## 3.4 Uhuishi

Uhuishi ni hali ya kuvipa vitu visivyo na uhai sifa na uwezo wa vitu vilivyo na uhai kwa mfano; binadamu ana uwezo wa; kuongea, kula na kucheka. Kwa mfano; tunaposema kuwa ‘jiwe lilitabasamu liliposikia mlio wa risasi’ jina ‘jiwe’ limehuishwa kwa sababu binadamu ambaye ana uhai ndiye aliye na uwezo wa kutabasamu na sio viumbe visivyo na uhai kama ‘mawe’. Tatachanganua namna mwandishi wa tamthilia hii ametumia uhuishi ili kuboreshaa kazi yake. Tutachanganua namna amedhihirisha au na kukiuka matumizi ya mikakati ya upole akizingaatia mbinu ya uhuishi.

Kwenye mazungumzo kati ya Siki na Waridi njaa imehuishwa kwa kupewa sifa ya kuwa na nguvu. Maneno yanayoonyesha uhuishi ni

54.“njaa ina nguvu imeangusha miamba”

Mwandishi alitumia uhuishi huu kurejelea wale wafanyakazi ambao walikuwa wamegoma kwa sababu ya kutolipwa mishahara yao, kucheleweshwa mishahara yao na kupewa mishahara duni. Mwandishi kupitia kwa mhusika Siki anazidi kusema kuwa njaa ina nguvu ya kuangusha miamba. Kama tujuavyo miamba ni vitu ambavyo haviwezi kuangushwa kutokana na nguvu zilizonazo. Katika muktadha huu miamba ni wale viongozi ambao wanaona kuwa wana nguvu na wanaweza kutumia nguvu zao kuangamiza wengine.

55. Siki: …Mimi nilimwambia!
Lakini wapi?
Watu wenye uwele
Na njaa vile vile
Wakusikilize wapi!
Njaa ina nguvu
Imeangusha miamba…

Uhuishi huu umetumika hivi kwamba wasomaji ndio wanaopata kutambua kuwa mwandishi alikuwa anarejelea njaa kuwa wafanyakazi na miamba kuwa viongozi. Kwa hivyo mkakati wa kuwa nje ya rekodi unaodai kuwa msemaji awasilishe maneno kwa njia ya moja kwa moja imedhihirika katika mazungumzo haya.

Aidha katika mazungumzo kati ya Siki na tatu kuna matumizi ya uhuishi. Katika mazungumzo yao wanahuisha neno mlango na kusema kuwa ‘mlango huenda ukasalimu amri’. Huu ni uhuishi kwa vile mlango hauwezi ukasalimu amri. Binadamu ambaye ni kiumbe aliye na uhai ndiye anaweza salimu amri. Kwa mfano,

56. Siki: ... mimi nitamwona nimwelezee tena.
Labda huenda Meya na wenzake
Wakaona umuhimu wake akiwaeleza.
Tatu: Nashukuru.
Siki: Nanyi vile vile msikate tama.
Endeleeni kushinikiza kumwona Meya.
Mlango hatimaye huenda ukasalimu amri.

Dida anapokuwa anafagia anaigiza kama askari wafanyavyo wakiwa na bunduki. Dida anasema kuwa ‘bunduki hutema risasi.’ Huu ni uhuishi kwa vile bunduki haiwezi ‘kutema’ Viumbe walio na uhai kama wanyama na binadamu ndio wanaoweza kutema kwani midomo yao huwa na mate.

Badala yake angesema kuwa bunduki hutoa risasi bali sio kutema. Maneno yanayodhihirisha upole katika muktadha wa mazungumzo ya Dida ni;

57.“Bunduki inayotema risasi tatu tatu”

Haya ni matumizi ya mkakati nje ya rekodi kwa kuwa hakuna uhusiano uliopo kati ya kutema na bunduki. Tabia inayohusishwa na bunduki sio tabia yake kwa kuwa kutema hakuna uhusiano wowote na bunduki.

58.Dida: (*Anaigiza sasa*)

Bunduki inayotema risasi tatu tatu
basi tena uwe umelala chini hivi.

Baadhi ya kanuni kama vile kanuni ya namna na idadi zilidhihirika katika matumizi ya mbinu hii. Hakuna uhusiano wowote uliopo baina ya yale yaliyokuwa yakizungumziwa na kile kinarejelewa. Kwa mfano, mwandishi anaposema kuwa wafanyakazi wakishinikiza kumwona Meya, mlango hatimaye utasalimu amri, hakuna uhusiano kati ya kumwona Meya na mlango kusalimu amri.

### 3.5 Methali

Methali ni mojawapo ya tamathali za usemi zinazotoa mafunzo ya hekima. Methali huwa na maana ya nje na maana ya ndani iliyo fiche. Kwa mfano, methali kama vile ‘ukitaka cha mvunguni sharti uiname’ ina maana kuwa mtu akitaka kitu ambacho ki mvunguni ni sharti ainame ndiposa aweze kufikia. Hii ni maana ya juu. Maana ya ndani au maana iliyo fiche ni kwamba, mtu akitaka kufanikiwa maishani ni lazima atie bidii na juhudi zake ndizo zitamfanya aweze kufanikiwa maishani.

Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*, mwandishi ametumia methali kadha wa kadha katika mazungumzo baina ya wahusika wake. Tutaweza kuchanganua iwapo methali hizi zilizingatia au na zilikiuka mikakati ya upole kulingana na Brown na Levinson (1987).

Katika mazungumzo kati ya Siki na Waridi, Siki anatumia methali ‘Ngoja ngoja huumiza matumbo’

59. Waridi: Mbona nisiwe na uhakika?
Siki: (*Kimya. Anaranda kwa kimya huku*

*ameshika kidevu chake.*) Waridi!
Waridi: Naam daktari!
Siki: Wakisubiri ugonjwa nao utasubiri?
Hujui ngaja ngoja huumiza
Matumbo?
Waridi: Haraka haraka haina Baraka.
Usisahau kuwa Mstahiki
Meya mwenyewe amesema.
Siki: Haya mazuri! Naona tuwashughulikie
wale ambao dawa za kuwafaa zipo….

Methali "haraka haraka haina Baraka" inadhihirisha matumizi ya kuwa ndani ya rekodi na wakati mwingine pia imedhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Hivi kwamba inatubidi tujue kile msemaji alidhamiria kusema ndiposa tunasema ni mkakati wa kuwa nje ya rekodi. Haya ni matumizi ya mkakati wa kuwa nje ya rekodi kwa vile katika muktadha wa mazungumzo haya, walikuwa wakirejelea dawa ambazo hazikuwa zimewasili. Wahusika hawakuwa wakirejelea matumbo ambayo yangeumizwa kwa kungoja sana bali walikuwa wanarejelea wanachenea hasa wale waliokuwa wagonjwa walioambiwa kuwa wangoje dawa zi baharini zitawasili baada ya wiki mbili. Aidha methali hii imedhihirisha matumizi ya mkakati nje ya rekodi kwa vile tunaona hali ambayo wanacheneo wanangoja kuwasili kwa dawa hizo. Methali hii imevunja kanuni ya uhusiano na imedhihirisha matumizi ya kanuni ya ubora na ukweli.

Katika ukurasa wa 12 hadi 13, Meya anatumia methali katika mazungumzo yao na Daktari Siki kuwa; 'Akili hii. Walisema ni mali.

60. Siki: Sivyo nisemsvyo. Ninalosema ni kuwa watu
wengi hawajaridhishwa
kwa namna mambo yanavyokwenda.
Meya: Huna habari kuwa walinichagua hao
hao watu? Mara ya ngapi hii
kunichagua? (*Akionyesha kwa vidole*.)
Tatu. Hata nikitaka nne, tano, na sita bado
watanipa. (*Akiashiria kichwa chake.)* Akili hii.
walisema ni mali. Kama unadhani kuwa
sina nitakuonyesha hivi
sasa. (*kimya*.) Nataka uone mwenyewe
udhibiti na ushawishi wa mambo ninaona….uk 12-13

Methali "akili hii walisema ni mali" imedhihirisha kanuni ya uhusiano inayodai kuwa msemaji aseme mambo yaliyo na uhusiano na mada wanayozungumzia. Imesemwa kwa namna iliyo sawa kabisa na hivyo ni kusema kuwa tunaweza kudhibitisha ukweli wa methali hii. Tutadhibitisha haya kwa kusema kuwa ndiposa mtu aweze kujiwekea mali ni sharti mtu huyo awe na akili timamu. Methali hii kwa hivyo imedhibitisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi.

Katika mazungumzo kati ya Diwani I na Meya, Diwani I anamwambia Meya kuwa 'yaliyopita yamepita. Tugange yajajo.'

61. Diwani I: Mimi nimempigia tangu juzi naye hapatikani.
Meya: Heri ningemsikiza Bwana Uchumi na Kazi.
Maneno yake sikuyapenda lakini naona yalikuwa na ukweli fulani.
Diwani I: Yaliyopita yamepita. Tugange yajayo.
Meya : Tutagangaje ya kesho bila kuganga ya sasa?

Kulingana na muktadha wa mazungumzo haya, methali " yaliyopita yamepita. Tugange yajayo" imetumika kuonyesha kuwa kila jambo lina wakati wake. Jambo likitendeka likapita hakuna haja ya kuanza kufikiria jambo hilo kwa vile tayari limepita. Inanekana kuwa Meya anajutia kutotii ushauri wa Diwani III ambao anaona ushauri wake ulikuwa wa ukweli na maana fulani kwake. Methali hii imedhihirisha matumizi ya kanuni ya uhusiano, ukweli na imesemwa kwa namna ifaayo. Kuna uhusiano wa karibu sana kuhusu yale Meya alishauriwa na yale anayojutia kwa sasa. Anajutia matendo yake ya kutomsikiza Diwani III na kuwa kama angemsikiza huenda yale yanayotendeka hayangekuwa yanatendeka wakati huo. Mkakati wa kuwa kwenye rekodi unaodai kuwa msemaji awasilishe ujumbe kwa msikilizaji bila kujali hali ya kuhifadhi uso wake umedhihirika katika matumizi ya methali hii kwa sababu ujumbe kwa Meya kutojali yaliyopita unamfikia Meya moja kwa moja bila kujali uso wake.

Katika ukurasa 45, Diwani III katika mazungumzo yao na Daktari Siki anatumia mdokezo wa methali, ' Lililoandikwa…' halifutiki.

63. .Siki: Sikuwa na hakika ya kukupata hapa.
Diwani III: Nende wapi bwana? Mji wenyewe ndio hivyo unavyouona.
Siki: Nilikuwa ninabahatisha na kumbe kubahatisha ndiko kupata.
Diwani III: Bahati ikisimama, imesimama...
Siki: Inasimama kama ya mtende.

Diwani III: Lililoandikwa…
Siki: Halifutiki kwa kweli. (*kimya.*) Kheri!
Diwani III: Naam! (Anamtazama.)

Methali "lililoandikwa…halifutiki" ina maaana kuwa jambo likiandikwa haliwezi futika na likifutika itajulikana kuwa tayari lilikuwa limeandikwa. Diwani III alitumia methali hii, kuonyesha kuwa ilikuwa imepangika kuwa yeye pamoja na Siki wangekutana na lazima ingekuwa hivo. Katika muktadha wa mazungumzo haya tutasema kuwa methali hii imezingatia matumizi ya mkakati wa kuwa nje ya rekodi unaodai kuwa msemaji awasilishe ujumbe kwa namna iliyo fiche au ya kimafumbo na msikilizaji aweze kutambua kile msemaji alidhamiria kumweleza kwa kuwa tunatambua kuwa hakuna jambo lililoweza kuandikwa bali ni ile hali ya Siki na Diwani III kupanga watakutana na ukweli wanakutana nyumbani kwa Diwani III. Kanuni ya uhusiano imekiukwa kwani hakuna uhusiano uliopo baina ya kile kilichoandikwa na kukutana kwa wawili hawa. Aidha kanuni ya namna imekiukwa kwani namna methali hii ilivyodokezwa haikuwa ya njia ya moja kwa moja**.**

### 3.6 Tashbihi

Tashbihi ni mbinu ya kulinganisha kitu kimoja na kingine kwa kutumia vihusishi na viunganishi kama vile; kama, mithili ya, mfano wa na ja. Katika mazungumzo kati ya Siki na Diwani III, Siki anasema kuwa yeye na Meya ni mfano wa mafuta na maji, 'mimi na Meya ni mfano wa mafuta na maji' UK 45

Tashbihi hii ina maana kuwa hata kama Siki na Meya ni ndugu wa toka nitoke, hawapatani. Tunafahamu kuwa maji kamwe hayawezi patana na mafuta. Meya kupitia uongozi wake anawadhalilisha wanacheneo. Siki anatetea haki zao kwa vile zimekiukwa na viongozi kama vile Meya mwenyewe, Diwani I, Diwani II na hata Bili. Tashbihi hii imekiuka kanuni ya uhusiano kwa vile hakuna uhusiano uliopo baina ya mafuta na maji na Meya na Siki. Kanuni ya idadi vile vile imekiukwa kwa kuwa maneno machache yametumiwa lakini hatuelewi ujumbe uliokuwa unapitishwa kwa wahusika.

Japo mwandishi ametumia maneno machache, hatuwezi kudhibitisha ukweli kuwa mafuta na maji ni vitu havipatani. Je, ni kwa kiasi gani au namna gani vitu hivi haviwezi patana. Kwa hivyo mkakati wa kuwa nje ya rekodi umethihirika katika tashbihi "mimi na Meya ni mfano wa mafuta

na maji” kwa kuwa hatuwezi tambua namna Siki na Meya hawapatani. Swali ni je, hawapatani kwa namna gani?

### 3.5 Hitimisho

Kupitia tamathali hizi za usemi, yaani, maswali ya balagha, sitiari, uhuishi, methali, tashbihi na majazi tumeona namna upole umedhihirika. Mikakati yote ya upole imeweza kudhihirika kupitia tamathali hizi za usemi.

# SURA YA NNE

# UPOLE NA UKUZAJI WA MAUDHUI KATIKA TAMTHILIA YA *MSTAHIKI MEYA*

## 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tunashughulikia jinsi upole unavyodhihirika ili kukuza maudhui kwa kutumia mikakati ya upole. Tunachunguza jinsi mikakati mbalimbali ya upole inavyotumiwa au inavyodhihirika ili kukuza maudhui. Tunachunguza namna mikakati ya upole kama ilivyopendekezwa na Brown na Levinson (1987) inavyokuza maudhui. Mikakati ya upole inayoshughulikiwa katika sehemu hii ni pamoja na, mkakati ndani ya rekodi, mkakati nje ya rekodi, mkakati hasi wa upole na mkakati chanya wa upole.

## 4.1 Mchango wa Mikakati ya Upole Katika Kukuza Maudhui

Utafiti huu unakusudiwa kuangalia namna upole unavyodhihirisha au na kukiuka mikakati ya upole ili kukuza maudhui kama vile; uongozi mbaya, ufisadi, ukoloni mamboleo, uongo n.k. Katika kufanya hivyo tumezingatia mikakati ya upole kama vile, mkakati ndani ya rekodi, mkakati nje ya rekodi, mkakati chanya wa upole na mkakati hasi wa upole.

### 4.1.1 Matumizi ya Mkakati Ndani ya Rekodi

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987: 68) mkakati wa ndani ya rekodi hulenga au hudhamiria kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji kwa njia iliyo toshelevu kabisa. Kinachosisitizwa zaidi na msemaji au mzungumzaji katika mkakati huu wa kuwa kwenye rekodi ni kuwasilisha ujumbe kwa msikilizaji. Msemaji huwa hana haja ya kuhifadhi uso wa msikilizaji. Msemaji anapotumia mkakati huu wa kuwa kwenye rekodi ni sharti ahakikishe kuwa ujumbe wake ni wa moja kwa moja na kwamba hauna utata wowote. Ujumbe ni sharti ueleweke kwa urahisi kwa sababu huwa hauhitaji ufafanuzi wowote.

Mkakati wa upole ndani ya rekodi huingiliana kabisa na kanuni za ushirikiano katika mazungumzo kama zilivyoelezwa na Grice (1975). Grice alisisitiza kuwa jukumu kuu la mzungumzaji au msemaji katika mawasiliano ni kuwasilisha ujumbe ulio kweli na ambao waweza thibitishwa. Aidha alisisitiza kuwa ujumbe uwasilishwe kwa namna ambayo itamfanya msikilizaji kuelewa haraka kwa vile ujumbe unaowasilishwa una uhusiano na mada inayozungumziwa. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* mkakati wa kuwa kwenye rekodi umedhihirika na kukuza maudhui kadhaa wa kadhaa.

Kwanza kabisa maudhui ya uongozi mbaya yamekuzwa kwa kutumia mkakati ndani ya rekodi. Uongozi mbaya ni uongozi usiotilia maanani masuala yanayoathiri wananchi na nchi kwa ujumla na baadaye husababisha uzoroteshaji wa uchumi na nchi na kupanda kwa gharama ya maisha. Maudhui haya yamekuzwa na mkakati wa kuwa kwenye rekodi kwa vile tunapata kudhihirisha uongozi mbaya kwa njia ya moja kwa moja na iliyo sahihi. Katika tamthilia hii uongozi mbaya umeendelezwa na wahusika kama vile Meya Sosi, Diwani I, Diwani II na Bili.

Meya Sosi ananyakua vipande vya ardhi vya umma na hata kumgawia rafikiye Bili. Anamweleza kuwa amebakiza vipande vitano incase.

64. Bili: …wewe bwana siku hizi lazima una pesa
licha ya hali ngumu.
Meya: Nisipokuwa nazo, nani atakuwa nazo?
Mimi nimeuza vipande vyangu
vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii.
Nimebakiza vitano incase.
Wewe nilikugawia vinne. Utaweza kuuza
kimoja au viwili kwa ajili hiyo. Vingine
viweke kwa ajili yao hao watoto
unaowahangaikia, hasa ile prime plot. (UK 47)

Katika mfano huu mkakati wa kuwa kwenye rekodi unaodai kuwa msemaji awasilishe ujumbe kwa msikilizaji kwa njia iliyo toshelevu kwa vile anasema wazi kile alichouza na ni vipande vya ardhi vitatu na kubakiza vitano incase.

Katika mazungumzo kati ya Bili na Meya, Meya anaposema “mimi nimeuza vipande vyangu vitatu vya ardhi kupata pesa…” maneno haya yanadhihirisha mkakati wa kuwa kwenye rekodi kwa kuwa tunafahamu wazi Meya ameuza vipande vya ardhi ya baraza na hivyo kuendeleza uongozi usiofaa.

Aidha Meya wa Cheneo anamwarifu Diwani III awaongeze madiwani mishahara ilhali wafanyakazi wa baraza la mji wa Cheneo wamegoma kwa sababu ya kulipwa mishahara duni na kutolipwa mishahara yao kwa wakati unaofaa.

**65.** Meya: Nashukuru kwa kuitikia wito wangu
mara moja.
Diwani III: Vizuri basi.
Meya: Jambo nililokuitia ni moja. Nalo ni hili.
Madiwani wetu wanahitaji
nyongeza ya mishahara mara moja na
ningependa nyongeza hiyo mpya
waipate katika malipo ya mwezi huu. (UK 52)

Kama kiongozi mwema Meya alitakikana kuwalipa wafanyakazi wa baraza la mji kwanza, anunue dawa zipelekwa hospitalini, aboresha hali ya maisha katika mji huo ndiposa aongeze mishahara ya madiwani. Katika mazungumzo haya maneno yanayodhihirisha matumizi ya kuwa kwenye rekodi ni "madiwani wetu wanahitaji nyongeza ya mishahara mara moja na ningependa nyongeza hiyo mpya waipate katika malipo ya mwezi huu." Maneno haya yamesemwa kwa njia iliyo wazi kabisa kwa kuwa tunafahamu madiwani wataongezwa mishahara kinyume na vile tulitarajia kuwa Meya atawalipa wafanyakazi mishahara yao.
Meya kwa upande mwingine anapendekeza wageni kutoka nchi za nje watakaotembelea mji wa Cheneo wanunuliwe mvinyo kutoka Urusi na divai kutoka Ufaransa. Kama meya wa baraza, alitakikana kutumia mamlaka yake ifaavyo na kununua vinywaji hivyo mjini cheneo ndiposa asitumie fedha nyingi za baraza kugharamia maandalizi ya wageni hao.

66. Meya: …La hasha! Mvinyo nitauagizia kutoka
Urusi na divai kutoka Ufaransa. Wale wa
kunywa wajue kuwa Cheneo si mji hivi hivi.
Wauone ukarimu wetu na maana ya udugu wetu…
Bili: (*Huku akielekea aliko Meya*) Aaah, bwana!
Furaha iliyoje kukutana na Mstahiki Meya! UK 25

Katika mazungumzo haya kati ya Meya na Bili, maneno yanayoonyesha matumizi ya kuwa kwenye rekodi ni "mvinyo nitaugiza kutoka urusi na divai kutoka ufaransa. Maneno haya yanadhihirisha kwa namna ya moja kwa moja kuwa Meya anatumia pesa za baraza la mji visivyo. Badala yake alifaa kununua vinywaji hivyo katika mji wa Cheneo.

Meya anapokosa kuboresha viwango vya elimu katika mji wa Cheneo anaendeleza uongozi mbaya.

67. Meya: Hata kidogo. Amekwenda ng'ambo kuwaonaa watoto
Wake. Siku ile nilikwambia hawasomei hapa tena.

Viwango viko chini kidogo.
Bili: Nakumbuka uliisha nitajia kuwa wangeenda kusomea ng'ambo.
Mpango mzuri.
Meya: Ndio hivyo bwana. Elimu yetu hapa ni ya kawaida mno.
Haina kubwa la kumfaa mtoto mwemye mzazi anayeona
Mbali.
Bili: (Anatabasamu) Kweli bwana. Ya kina yakhe hii. (Kimya.)
Vipi mama? Hivi alishapata mgeni au vipi?
Meya: Bado. Karibuni.
Bili: (Kwa bashasha.) Mara ile ya mwisho tulipokuwa pamoja
Alionekana amechoka sana!
Meya: Ndio maana alisafiri ng'ambo. Madaktari wetu hawa wa
kubahatisha ti. Kule ng'ambo ndipo walipo wakunga
wenyewe…. UK 26-27

Katika mazungumzo haya kati ya Meya na Bili, maneno yafuatayo yanadhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi.

68. "…elimu yetu hapa ni ya kawaida mno. Haina kubwa la kumfaa mtoto mwenye mzazi anayeona mbali"

Katika mazungumzo haya ni wazi kuwa Meya hathamini viwango vya elimu katika Cheneo ndiposa anapeleka watoto wake ng'ambo kusomea huko. Hata hivyo, tunatarajia kama kiongozi aboreshe viwango hivyo ambavyo ni duni. Kipengele kingine kinachodhihirisha matumizi ya mkakati ndani ya rekodi ni;

69. "…ndio maana alisafiri ng'ambo. Madaktari wetu hawa wa kubahatisha tu."

Katika muktadha wa mazungumzo haya ni wazi kuwa viwango vya afya katika Cheneo si bora. Kusafari ng'ambo ina maana kuwa anataka kupata matibabu yaliyo bora bora kuliko yale ya mji wa Cheneo.

Maudhui mengine yanayodhihirisha matumizi ya mkakati ndani ya rekodi ni utetezi wa haki. Ni wajibu wa kila mwananchi kuwa na haki zake za kuishi. Katika jamii hii ya Cheneo, wale wanaodhulumiwa ni wale maskini kwa vile wanaowadhulumu wanafikiria kuwa maskini hana haki. Wanaodhulumiwa wanatumia mbinu mbalimbali ili kutetea haki zao. Wawakilishi wa wafanyakazi wanatumiwa ili kutetea haki zao lakini haya yote yanagonga mwamba. Wahusika wanaosaidia kutetea haki za wanyonge ni kama vile; Diwani III, Siki, Tatu, Beka na Medi ambao ni wawakilishi wa wafanyakazi. Diwani III anasisitiza mipango ya kuwanufaisha watu kwa mahitaji kama vile elimu na malipo bora kwa wafanyakazi. Hii ndio sababu kuu kuwa anatetea

haki za wafanyakazi wa baraza la mji kwa kutaka Meya awalipe mishahara yao badala ya kuongeza madiwani mishahara.

Siki anaenda kwa Meya ili kutetea haki za wanyonge. Katika kutetea haki hizi anamwelezea Meya matokeo ya uongozi wake. Hivi kwamba hatetei haki za waliomchagua kwa kuwa kila uchao, hali ya maisha ya wanacheneo inaendelea kuzorota. Maudhui haya yalidhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa ndani ya rekodi kwa vile tunaona moja kwa moja vile wakombozi hawa, yaani, Siki, Diwani III na wawakilishi wa wafanyakazi.

Maudhui ya dhuluma yaamedhihirika kupitia mkakati wa kuwa kwenye rekodi unaodai kuwa msemaji awasilishe ujumbe wake kwa njia ya moja kwa moja bila kujali uso wa msikilizaji. Dhuluma ni hali ya kumnyanyasa mtu au kumtesa mtu kiasi cha kumnyima mtu huyo haki yake. Maudhui haya yamedhihirika kupitia kwa mkakati wa kuwa kwenye rekodi kwa vile matendo yanayotendewa wadhulumiwa yanadhihirika moja kwa moja. Matendo haya yanaonyesha wazi unyanyasaji unaotendewa wafanyakazi wa baraza la mji wa cheneo.

Kwanza kabisa wanyonge wanapuuzwa kwa kukosa lishe bora. Ukosefu wa lishe bora ndio uliosababisha mama yake Dadavuo Kaole kumlisha mwanawe chakula cha mbwa kilichokuwa kimelala.

70. Siki: Jina?
Mama: Dadavuo Kaole
Siki: Umri?
Mama: Miaka mitatu.
Siki: (Akimtazama mama.) Ulimlisha nini?
Mama: Chakula.
Siki: (Ameelekea kuudhika.) Chakula gani?
Mama: Nilichotoa kwa bwana.
Siki: (Akimtazama.) Kwa bwana?
Mama: Eeh! Ninakofanya kazi.
Siki: Unafanya kazi wapi?
Mama: Kwa Mstahiki Meya.
(Kimya cha muda)
Waridi: Chakula gani hicho hasa ulichochukua kumpa mtoto?
Mama: Wali na maharagwe yalolala.
Siki: Wewe hukuyala?
Mama: Sikuyala mie. Yalikuwa machache tu! Uk 4-5

Maneno yanayodhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi ni

71. “wali na maharagwe yalolala.”

Maneno haya yamedhihirisha kwa namna iliyo wazi kuwa kula wali na maharagwe yalolala bila kuchemsha ni hali ya kuwa katika umaskini. Umaskini huu umejitokeza kwa njia iliyo wazi na ya moja kwa moja. Chakula hicho hakikuwa kimechemshwa kwa sababu ya ukosefu wa mafuta ya taa. Ulaji wa chakula cha mbwa ni dhuluma kwa vile katika jamii zetu, mbwa ni mnyama ambaye hathaminiwi. Dhuluma hii imejitokeza kwa njia iliyo wazi kwa hivyo mkakati wa kuwa kwenye rekodi unaodai kuwa mawasiliano yawe ya moja kwa moja ili yaeleweke vyema bila matatizo yoyote umedhihirika. Katika mazungumzo kati ya Mamake Dadavuo na Daktari Siki mkakati huu unadhihirika wazi kabisa.

Wakati wafanyakazi wa baraza la mji wa cheneo wanapogoma, wanatishwa kuachishwa kazi na kuajiri wengine. Hii ni dhuluma kwa sababu badala ya Meya kusikiliza malalamishi ya wanacheneo na kuwaalipa mishahara yao, anawatisha kwa kusema kuwa atawafuta kati. Meya hana haja ya kuokoa uso wa wafanyakazi kwa kuwa anawatolea vitisho kwa njia iliyo wazi kuwa atawafuta kazi wakiendelea kugoma na ajiri wafanyakazi wengine. Huu ni mkakati wa kuwaa kwenye rekodi. Kumfuta mtu kazi wakati ambapo anadai haki yake ni kitendo cha dhuluma.

Wananchi wanyonge walinyimwa huduma bora ya matibabu kwa sababu hakukuwa na dawa hospitalini. Dawa zilizopatikana hospitalini zilikuwa ni zile za kupunguza na kudhibiti maumivu.

Maudhui mengine ambayo yanadhihirika kupitia mkakati wa kuwa kwenye rekodi ni usaliti. Usaliti ni hali ya mtu kutenda au kufanya jambo fulani kinyume na vile jamii ilitarajia. Kwa mfano, wanajamii wanapochagua viongozi, kama vile wabunge, maseneta, n.k wanatarajia kiongozi huyo awasaidie na askize malamishi yao. Kiongozi anapokosa kuwajibiki anawasiliti wananchi.

Diwani I, Diwani II na Meya wanamsaliti Diwani III. Licha ya yeye kuwa mmoja wa wanakamati katika baraza la mji wa Cheneo, hawamhusishi katika mipango na mikutano yote ya baraza la mji huo. Kwa mfano, wanaamua kuwa, madiwani wote wasitozwe kodi, ilhali, mama

muuza mboga analipa kodi. Aidha wanashirikiana na Meya katika mpango wakuongezea madiwani mishahara bila kumhusisha Diwani III.

Mstahiki Meya anawasaliti wananchi wa mji wa Cheneo waliomchagua. Anawasaliti kwa kutoweka dawa hospitalini. Gharama ya matibabu pia ni ghali mno na wananchi hawawezi mudu gharama hizo kwa sababu ya umaskini unaotokana na hali ya maisha kwenda juu. Katika mfano huu, Meya pamoja na baraza lake wamewasaliti wananchi.

72. Waridi: Tukae tu na kungoja. Nao wakisubiri.
Wenye kulazwa nao na walipie!
Siki: Walipie kitanda kisicho dawa?
Waridi: Si zimo njiani!
Siki: Njiani ni njiani na hospitalini ni hospitalini.
Meya wetu anaweza kusema chochote mradi
anaona kuwa kitaonyesha kuwa Baraza
linajitahidi kuwajibikia. Zake huwa ni kauli
zinazoanguliwa katika matamshi….uk 6-7

Katika muktadha wa mazungumzo haya, maneno yanayodhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa kwenye rekodi ni;

73. "Walipie kitanda kisicho dawa?"

Maneno haya yanadhihirisha maudhui ya usaliti kwa vile ni wazi kuwa Meya amewasaliti wanacheneo kwa kutoweka dawa hospitalini na anataka wanacheneo walipie gharama zote za matibabu bila kupewa dawa naakuhudumiwa ipasavyo.

### 4.1.2 Matumizi ya Mkakati Hasi wa Upole

Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1987:129), mkakati hasi wa upole hutumiwa ili kuutambulisha uso hasi wa msikilizaji kwa kuonyesha tofauti iliyopo baina ya msemaji na msikilizaji. Kwa kuwa msemaji atakuwa analazimisha matamanio yake kwa msikilizaji, basi kuna uwezo mkubwa wa kumwaibisha. Msemaji anaweza kumwaibisha msikilizaji kwa kumwomba vitu kwa lazima, kumtuma kufanya kazi na hakuwa anataka kufanya kazi hiyo na hata kumtembelea mtu bila idhini yake. Maudhui yafuatayo yamedhihirika kupitia kwa mkakati hasi wa upole.

Katika mazungumzo kati ya Meya na Bili maudhui ya ufisadi yamedhihirika kupitia mkakati hasi wa upole. Ufisadi ni hali ya kutumia mali au fedha za umma visivyostahili ili kujinufaisha.

Ufisadi pia unaweza dhihirika kupitia kwa kutoa hongo au mlungula ili upate kufanyiwa jambo fulani ambalo hungepata kufanyiwa kwa njia ifaayo ya kawaida iliyo wazi.

Meya na rafikiye Bili wanaungana kwenda kujivinjari katika hoteli ya kifahari wakitumia pesa ya umma. Kwa mfano,

74. Meya: Ndiyo hivyo bwana. Muhimu.(Kimya.)
Vipi nyumbani? Wote wazima lakini?
Bili: Wazima. Hawaishi kuizungumzia siku ile
huko Kajifahari. Bado najiandaa halafu
nitakuomba uje na Memsahib na watoto
ili tukajinafasi.

Katika mazungumzo haya kati ya Meya na Bili, maneno yanayoonyesha mkakati hasi wa upole ni;

75. " Bado najianda halafu nitakuomba uje na Memsahib na watoto ili tukajinafasi"

Bili anaposema maneno haya, Meya anamjibu kuwa,

76. " kama wanataka wewe walete tu. Kila kitu juu yangu. Nina entertainment vote"

Kwa kuwa Bili analazimisha matamanio yake kwa Meya, Meye atakubali matamanio yake kwa kutotaka kumwaibisha ndiposa anamwalika Bili pamoja na familia yake katika hoteli ya Kajifahari ndiposa asiuaibishe uso hasi wake.

Mwandishi ametumia mkakati hasi wa upole kudhihirisha maudhui haya. Hivi kwamba Meya na Bili kujivinjari katika hoteli ya Kajifahari pamoja na familia zao inaonyesha matumizi mabaya ya fedha au pesa za umma na hii inadhihirisha maudhui ya ufisadi. Uso hasi wa wanacheneo unaaibishwa kwa kuwanyanyasa wakitumia pesa na mali ya baraza visivyo.

Meya anaidhinisha malipo kwa Bili ambaye si mfanyakazi wa baraza la Cheneo na kukubali malipo ya 'overtime' kwa Diwani I na Diwani II.

77. Diwani I: Labda marupurupu kidogo Mstahiki Meya.
Diwani II: Overtime labda.
Meya: Bili je? Si mfanyakazi wa baraza la mji!
Diwani II: Anaweza kulipwa kwa huduma za ushauri
kwa Baraza.UK 61

Katika muktadhaa wa mazungumzo haya, Meya anaidhinisha malipo kwa Bili ndiposa asiudhuru uso hasi wake. Maneno yanayodhihirisha mkakatihasi wa upole ni;

78. "Anaweza kulipwa kwa huduma za ushauri kwa Baraza"

Huu ni ufisadi kwa kuwa watakuwa wanatumia pesa za Baraza visivyo kulipa mtu ambaye sio mfanyakazi wa baraza. Meya anafanya hivyo ili kuhifadhi uso hasi wa Bili, asiudhuru kwa vile ni rafikiye.

Bili, Meya, Diwani I na Diwani II wanafisadi baraza la mji wa Cheneo kwa kuiba fimbo ya Meya na kuitaftia soko ng'ambo. Kuuza kwa fimbo ya Meya kunadhihirisha mkakati wa kutaka kuokoa uso hasi kwa vile hawatataka mtu yeyote atambue kile walichokitenda. Wanapanga kuwa iwe njama yao ndiposa pesa zitakazopatikana ziwe zao.

79. Meya: Bila shaka sisi. Haya leta mpango Bili.
Bili: Fimbo ya Meya ipo?
Meya: Fimbo ipo.
Bili: Si hiyo dhahabu tupu? Kwa nini ubebe
Dhahabu mkononi kana kwamba ni tope?
Meya: Ni kanuni ya umeya.
Bili: Mtu hali kanuni Mstahiki Meya!
tunaweza kuitaftiaa soko ng'ambo. Tena
Bei nzuri. UK 61-62

Katika mfano huu, Meya antumia mkakati hasi wa upole anapomwamuru Bili kuleta mpango.

80. "Haya leta mpango Bili." Kisha Bili anajibu

81. "Fimbo ya Meya ipo"

Maneno haya yanadhihirisha mkakati hasi wa upole kwa kuwa Meya anataka watafute namna nyingine ya kupata pesa ndiposa rafikiye awe na pesa.

### 4.1.3 Matumizi ya Mkakati Chanya wa Upole

Kulingana na Brown na Levinson (1987:101), mkakati chanya wa upole hutumika na msemaji kwa msikilizaji ili kumwonyesha kuwa anamjali kwa kushughulikia uso wake chanya. Msemaji

hushughulikia uso chanya wa msikilizaji kwa kumheshimu, kutombagua hata kama ana ulemavu wa kimaumbile na kutomjulisha mambo muhimu katika jamii. Kwa misingi hii, msemaji huufurahisha uso chanya wa msikilizaji kwa kumjengea mazingira mazzuri wakati wa mazungumzo na kuonyesha uhusiano mwema baina yake na msikilizaji.

Katika mazungumzo nya washirika, mkakati chanya wa upole huweza kudhihirishwakatika mazungumzo ya washirika kupitia kwa matumizi ya mbinu mbalimbali. Baadhi ya mbinu hizi ni pamoja na, kuyajali maslahi ya msikilizaji, kukabiliana na maoni ya wasikilizaji, kumtolea msikilizaji ahadi, kujitambulisha pamoja na msikilizaji na kumwonyesha msikilizaji huruma. Mbinu hizi zisipozingatiwa na msemaji wakati wa mazungumzo, basi msemaji atakuwa amekiuka mkakati chanya wa upole ambao hudaai kuwa katika mazungumzo ni sharti msemaji anapozungumza na msikilizaji afanye hivyo kwa njia inayoonyesha kuwa anamjali.

Brown na Levinson (1987), wanadai kuwa, mkakati huu hutumika katika mazungumzo miongoni mwa watu wanaofahamiana sana au watu ambao ni marafiki. Aidha mkakati huu huweza kutumiwa na watu walio na ukaribu miongoni mwao kama watu wa familia moja au wafanyikazi. Watu hawa watazingatia mkakati huu wakati wa mazungumzo yao kwa sababu hawatataka kuwaaibisha watu walio karibu nao. Katika utafiti wetu tumeweza kuona namna mkakati huu umekiukwa ili kukuza baadhi ya maudhui katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*.

Maudhui ya kwanza ni umaskini. Umaskini ni hali ya kutokuwa na uwezo wa kumudu mahitaji ya kimsingi ya maisha. Maudhui haya yanadhihirika kupitia kwa mamake Dadavuo Kaole. Mama huyu alikosa chakula cha kumpa mwanawe na ikabidi akile chakula kilichopimiwa mbwa na makombo yaliyobaki kwa Meya. Badala ya Meya kumpa mamake Dadavuo Kaole chakula, anamwacha akile chakula kilichowekewa mbwa. Meya hajali maslahi ya wanacheneo.

Zahanati katika mji wa Cheneo haikuweza kumudu vijitabu au hata karatasi za kunakili udodosi. Hospitali hazikuwa na dawa za kuwatibu wagonjwa. Kutokana na umaskini wananchi hawawezi mudu gharama za maisha. Wananchi wengi waliaga kwa kukosa kumudu gharama za matibabu kutokana na umaskini.

Wafanyakazi wa baraza la mji wa Cheneo walifanya kazi kwa mazingira duni kwa mfano, waliosha vyoo bila glavu. Wafanyakazi wa baraza la mji walishindwa kukopa bidhaa kwa kuwa walikuwa na wasiwasi kuwa wangekosa kulipia bidhaa hizo wakati ufaao.

Aidha watoto wa maskini wanaenda shule kwa miguu. Hii ni kinyume na watoto wa matajiri wanaosomea shule za ng'ambo na wale wanaosomea mji wa Cheneo wanapelekwa shuleni na kurudishwa wakitumia magari za baraza la mji.

Kupitia maudhui haya tuliona namna mwandishi alivyokiuka baadhi tu ya kanuni za upole kama vile upole hasi, upole chanya na mkakati wa kuwa kwenye rekodi. Hata hivyo, katika utafiti wetu tuliweza kuchanganua namna maudhui haya yalivyodhihirika tukitumia kanuni ya namna na kanuni ya uhusiano. Kwa mfano, tulichanganua namna umaskini ulivyo na uhusiano na kwenda shule za kiwango cha chini kwa vile huwezi mudu gharama ya shule za viwango vya juu. Aidha tuliweza kuchanganua uhusiano uliopo baina ya umaskini na kutomudu bidhaa muhimu katika maisha kama vile chakula. Kwa hivyo umaskini umedhihirisha mikakati ya upole kama vile mkakati chanya wa upole.

Maudhui mengine yanayodhihirisha ukiushi wa mkakati chanya wa upole ni ukoloni mamboleo. Ukoloni mamboleo ni hali ya viongozi wa kiafrika kuendeleza unyanyasaji dhidi ya watawaliwa hata baada ya kujinyakulia uhuru kutoka kwa wazungu. Hali hii husababisha wananchi kuteseka kama walivyoteseka wakati na kabla ya kujinyakulia uhuru. Sera za kiongozi wa cheneo zimejikita katika mfumo wa wakoloni waliotoweka. Maudhui haya yamejidhihirisha kupitia kwa mambo kama vile mfumo wa elimu, bidhaa zitumiwazo na wananchi, kiuchumi na hata kisiasa.

### 4.1.4 Matumizi ya Mkakati Nje ya Rekodi

Brown na Levinson (1987:211) wanaeleza kuwa, mkakati wa kuwa nje ya rekodi hukabiliwa na hatari ya ufasili potovu wa maana na msikilizaji kwa vile huwa si wa moja kwa moja. Kulingana na Brown na Levinson, mkakati huu huvunja kanuni za utaratibu wa ushirikiano kama zinavyopendekezwa na Grice (1975). Kwa msingi huu msikilizaji hutarajiwa kuwa na ufahamu wa awali kuhusu kile kinachorejelewa na msemaji. Katika kutumia mkakati huu wa upole nje ya rekodi, msemaji hulazimika kuwasilisaha ujumbe wake kwa msikilizaji kwa njia isiyo ya moja

kwa moja. Kwa hivyo msingi wa mkakati huu ni uelewa na ufasili wa maana wa msikilizaji katika kufaafanua kinachosemwa.

Katika mazungumzo kati ya mhubiri na Meya, Mhubiri anaisaliti imani yake ya dini anapomsifu Meya licha ya uongozi wake mbaya badala ya kumkosoa. Mhubiri alitakiwa kuukashifu uongozi wa Meya uliojaa dosari chungu nzima.

82. Mhubiri: Ni furaha yangu kuona wanasiasa kama
Wewe wakiutafuta upendo wa bwana.
(*Sauti inazidi kupanda*) Uongozi unaotafuta
Dini utadumu maana umebarikiwa
Meya: Ameeen! (*Kimya*) Natuombe mpendwa wa bwana…UK 41-42

Katika muktadha wa mazungumzo haya kipengele kinachoonyesha matumizi ya mkakati ndani ya rekodi ni;

"Ni furaha yangu kuona wanasiasa kama wewe wakiutafuta upendo wabwana"

**4.2 Hitimisho**

Katika sura hii tuliweza kuona namna upole unavyodhihirisha ili kukuza maudhui. Mwandishi kupitia kwa wahusika wake ameweza kukiuka mikakati kadha ya upole kama vile; mkakati wa upole hasi na mkakati wa upole chanya. Hivyo basi mikakati hii ya upole imesaidia katika kukuza maudhui kwa jumla.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Katika utafiti huu tumeshughulikia mikakati ya upole katika tamthilia ya Mstahiki Meya kwa kutumia nadharia ya upole. Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa kutathmini namna mwandishi alivyotumia tamathali za usemi kwa kuzingatia mikakati ya upole na ulinuia pia kubainisha namna upole unavyodhihirika ili kukuza maudhui.

Tuliweza kuchunguza mikakati ya upole kama vile; mkakati wa upole hasi, mkakati wa upole chanya, mkakati wa kuwa ndani ya rekodi, mkakati wa kuwa nje ya rekodi na mkakati wa kutowasilisha ujumbe wowote. Tuliweza kuchanganua tamathali za usemi zilizodhihirisha na kukiuka upole. Kwa kiasi fulani tuliweza kugundua kuwa tamthilia ya Mstahiki Meya imekiuka baadhi ya mikakati ya upole iliyokuwa ikichunguzwa katika utafiti huu kama vile; mkakati wa kutowasilisha ujumbe wowote. Wahusika katika tamthilia hii hawajadhihirisha matumizi ya mkakati wa kutowasilisha ujumbe wowote.

Sura hii inatoaa muhtasari wa matokeo na kufafanua iwapo malengo yetu yaliafikiwa au la. Aidha tutatoa mapendekezo kuhusu tafiti zijazo kuhusu suala la upole katika tamthilia kwa jumla.

## 5.1 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Katika sura ya kwanza tulibaini tatizo letu la utafiti na maswali yaliyonuiwa kutusaidia kuchanganua kazi yetu. Tuliweza kubaini malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa kinadharia ambapo tuliweza kubaini mikakati mbalimbali ya nadharia ya upole, yaliyoandikwa kuhusu Nadharia ya Upole na mwisho mbinu za utafiti wetu.

Katika sura ya pili ya utafiti huu, tulieleza dhana ya upole kwa upana kulingana na baadhi tu ya waasisi wa nadharia hii. Tulichanganua mawazo ya Grice (1975), Leech (1983) na Brown na Levinson. Tuliweza kutoa maelezo mbalimbali kuhusu alivyopendekeza Grice (1975) kuwa kuna kanuni nne za upole, yaani; kanuni ya idadi, kanuni ya namna, kanuni ya uhusiano na kanuni ya maneno ambayo wanaweza dhibitisha ukweli wake, maneno hayo lazima yawe na uhusiano nay ale wanayozungumza, wawasiliane kwa namna bora na wasipujiane nyuso na mwisho waseme

maneno machache yanayoweza kueleweka kwa urahisi. Pia tulichanganua kaida za Leech (1983) ambapo alipendekeza kuwa wakati wa mawasiliano msemaji ni sharti awe mkarimu kwa msikilizaji, aonyeshe huruma kwa msikilizaji, amsifu msikilizaji, ajitweze na awe na makubaliano na msikilizaji katika mazungumzo yao. Tuliweza kugundua kuwa kuwa kaida hizi za Leech (1983) zilikuwa na gharama kwa msemaji kuliko ilivyokuwa kwa msikilizaji. Katika sura hii pia tuliweza kuchanganua Nadharia ya Upole kulingana na Brown na Levinson (1978) ambapo walipendekeza namna ya kukabiliana na vitendo vinavyotishia uso na mkakati wa kuwa nd. Walipendekeza namna kama vile; mkakati chanya wa upole,mkakati hasi wa upole, mkakati wa kuwa nje ya rekodi.

Katika sura ya tatu tulichanganua mikakati ya upole kwa kujikita katika kipengele cha tamathali za usemi katika tamthilia ya *Mstahiki Meya.* Tamathali tulizochunguza ni kama vile; majazi sitiari, maswali balagha na uhuishi. Katika kuzingatia tamathali hizi tulieleza iwapo mwandishi alikiuka na alidhihirisha matumizi ya mikakati ya upole. Tuligundua kuwa kulikuwa na hali ya kuchanganua tamathali moja ya usemi kwa kutumia mikakati zaidi ya moja. Kwa mfano, tamathali kama vile methali ilichanganuliwa na mikakati kama vile, mkakati wa kuwa nje ya rekodi, ndani ya rekodi na hata kanuni za ushirikiano za Grice (1975) kama vile kanuni ya uhusiano na kanuni ya ukweli. Kuna baadhi ya methali aambazo zimedhihirisha ukweli fulani na zile ambazo zina uhusiano na yale ambayo yanasemwa.

Hali hii imetokea wakati ambapo maana ya methali inachanganuliwa na pia kujaribu kuchanganua kile mwandishi alidhamiria kusema. Tulijaribu kukabiliana na changamoto hii kwa kuangazia mikakati hii yote inavyojitokeza katika kila tamathali ya usemi. Tamathali nyingi za usemi zimedhihirisha matumizi ya mkakati wa kuwa nje ya rekodi kwa hivyo imebidi tuchanganue kiundani kabisa ndiposa kufahamu kile mwandishi alidhamiria kusema.

Katika sura ya nne tulichanganua namna upole hudhihirika katika ukuzaji wa maudhui.

## 5.2 Hitimisho

Katika sura hii tumeangalia muhtasari wa matokeo ya utafiti. Tumeshughulikia namna upole unavyoweza kudhihirisha au kukuza maudhui na namna tamathali za usemi zinavyoendeleza upole.

## 5.3 Mapendekezo Kuhusu Tafiti Zijazo

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tuligundua kuwa upole ni dhana pana ambayo inaweza kutafitiwa. Tafiti za baadaye zinaweza chunguza namna mikakati ya upole inavyotumiwa na wahusika wakuu na wahusika wasaidiki au wadogo katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Vile vile, tungependekeza utafiti zaidi kuhusu mikakati ya upole katika tamthilia nyinginezo za Kiswahili. Aidha tafiti za baadaye pia zinaweza chunguza namna wahusika wanavyojengwa kwa kukiuka au na kudhihirisha upole.

## MAREJELEO


Arege, T (2009) *Mstahiki Meya.* Nairobi: Vide Muwa Publishers Limited**.**

________ (2009) *Kijiba cha Moyo*. Nairobi: Longhorn Publishers

Brown, P. na Levinson, S. (1987) *Some Universal in Politeness Usage*. Cambridge: Cambridge University press.

Brown, P na G.Yule (1983) *Discourse Analysis.*Cambridge: Cambridge University Press.

Buliba, A., Njogu, K. na Mwihaki, A. (2006). *Isimujamii kwa Wanafunzi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Cartes na Mocarthy (1994). *Language as discovered perspective for language teacher*. New York, Longman.

Coates, J. (1986).*Women Men and Language.*UK: Essex Longman Group Limited.

Coyle, C. et al, (1991). *Encyclopedia of Literature and Criticism*. London: Macmillan

Gadzar, G. (1979). *Pragmatics*: *Implicature, Presupposition and Logical Form*. New York: Academic Press.

Gennette, G. (1972) *Narratology.* Imesemwa (Jumapili 08/0/|2015 saa 2.00pm) http://www.signosemio.com/genette/narratology.asp

Gennette, G. (1980) *Narrative Discourse.* Ithaca: Cornell University Press

Goofman, E. (1967). *The presentation of self in everyday life*: Basic Books New York

Goofman E, (1971). *Relations in public: Microstudies of the public order:* Basic Books:New York

Grice, H. P. (1975). *Logic and Conversation: Philosophy of Language.* New York: Oxford University Press.

Guinner, L. (1998). *Life as a female Gentleman in exploring Language na Goshgarian 8th edition.* US: Addison Wesley Education Publisher.

Habwe, J. (2010). *Swahili Forum 17: Politeness Phenomena*: *A Case of Kiswahili Honorifics*.

Hussein, E. (1971) *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press

Kaui, T. (2012) *Mwongozo wa Mstahiki Meya*. Nairobi: Queenex Publishers

Kimani, P. (2012) "Arki za simulizi katika utendi wa Mikidadi na Mayasa" Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

King'ei, G. etal (2012) *Mwongozo wa Mstahiki Meya* (Timothy M. Arege) Nairobi: Target Publishers

Lackoff, R. (1976). *Language and Society in a Survey of Applied Linguistics.* Michigan: University of Michigan Press.

Leech, G. (1983). *Principles of Politeness*. London: Longman Publishers.

Marmaridou, S. A. (2000). *Pragmatic, meaning and cognition,* Amsterdam: John Benjamins publishing company.

Mbuthia, E. (2012) *Mwongozo Changanuzi wa Mstahiki Meya.* Nairobi: Target Publishers

Mbuvi, F. na Were, E. (2012) *Mwongozo Changanuzi wa Mstahiki Meya*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers

Mjomba, G. (2015) " Uchambuzi wa nyimbo za Harusi za Wadawida." Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Mugenda na Mugenda. (1999). *Research Methods*: Quantitative and Qualitative Approaches. Nairobi: Act press.

Muturi, M. (2012) *Mwongozo wa Mstahiki Meya* (Timothy Arege). Nairobi: Top Achievers Publishers

Ndege, C. (2013) Ukuaji wa muundo katika tamthilia za Arege: Mtazamo wa Muundo. Tasnifu ya M.A. Chuo kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Okwena, S. (2013) “*Matumizi ya Jazanda katika tamthilia tatu za Timothy Arege: Mtazamo wa Muundo.*” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta (Haijachapishwa)

Owini, N. (2010) *Uchanganuzi wa matini teule wa nyimbo za Foustine Munishi kwa misingi ya nadharia ya upole*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Raitania, A. (2014) “*Mikakati ya upole katika vipindi vya Runinga: Mawaidha na Bi. Msafwari katika Runinga ya Citizen*” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Nairobi (Haijachapishwa)

Trudgil,P. (1883) *Sociolinguistics. An introduction to Language and Society (3rd Edition)* London: Pinguin Books

Wafula, R. na Kimani, N. (2007). *Nadharia za uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation

Walubengo, G. (2010) “*Swala la upole katika nyimbo za Sherehe za jando za jamii ya Wabukusu.* ” Tasnifu ya Uzamili ya M.A. ya Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: focus publishers.

______________(2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: vide-Muwa Publishers.